# Nipashe

Alhamisi Mei 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580957

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Spika:** Kulia bungeni ruksa sarakasi hapana

UKURASA 4



## BENZEMA AKANA KUMUITA MBAPPE MSALITI MADRID

UKURASA 22



Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi



Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia

# Sakata Mbatia, Msajili laingia ukurasa mpya

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**BABA NA MWANAWE KUNYONGWA HADI KUFA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Musoma kupitia Mahakama ya Wilaya Tarime...

UKURASA WA 5

**CHONGOLO ATAJA MWAROBAINI WA UTATUZI WA AJIRA AFRIKA**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ame...


# Meneja stendi Magufuli azomewa ziara viongozi wa CCM

UKURASA 4




UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan, akionyesha Tuzo ya Babacar Ndiaye 2022, aliyoipata kutokana na mafanikio kwenye ujenzi wa barabara, baada ya kukabidhiwa na Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Solomon Quaynor (kushoto), jijini Accra, nchini Ghana jana. **PICHA: IKULU**



# Samia amtaja JPM tuzo ubora Afrika

**MICHEZO** YANGA: WAJE TU, SISI TUPO TAYARI UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akizungumza wakati wa majadiliano maalum ya Viongozi Wakuu wa Nchi za Afrika katika ajenda ya namna Bara la Afrika linavyoweza kubadili utaratibu wa kimataifa katika kukabiliana na masuala mbalimbali, uliofanyika katika mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani unaoendelea Davos, nchini Uswisi jana. Kulia ni Rais wa Rwanda, Paul Kagame. **PICHA: OMR**

# Sakata Mbatia, Msajili laingia ukurasa mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikitangaza kubariki uamuzi wa kusimamishwa kwa Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, mwenyewe ameibuka na kutangaza kuwa uamuzi dhidi yake ni batili.

Mapema jana, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ilitangaza kubariki uamuzi wa kusimamishwa kwa Mbatia na sekretarieti yake yote kujihusisha na siasa ndani ya chama hicho hadi uamuzi huo utakapoamuliwa vinginevyo.

Hata hivyo, akizungumza na waandishi wahabari jana mkoani Dar es Salaam muda mfupi baada ya taarifa kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Mbatia alisema yeye bado ni mwenyekiti halali wa chama hicho na kikao kilichofanyika cha kumng'oa hakikuwa halali.

Mbatia alisema: "Mimi bado mwenyekiti halali wa NCCR-Mageuzi kwa mujibu wa katiba na taratibu zote za nchi, hata Katiba ya NCCR-Mageuzi. Hapa kuna ajenda fiche."

Pasi na kuweka wazi alichokiita ajenda fiche, Mbatia alisema kikao kilichofanyika kwa lengo la kumng'oa madarakani, hakikufuata taratibu, kikitumia dakika 40 kupitisha ajenda zaidi ya nne licha ya Kaimu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, kubariki uamuzi wa kikao hicho.

"Kaimu Msajili anasema kikao kilikuwa halali, kipi hicho? Hata Makamu Mwenyekiti wangu hakuwa na taarifa, Hata Kaimu Katibu Mkuu wa chama hana taarifa. Haya yote yanayotokea ni mazingaombwe," alisema Mbatia.

Alidai kuwa yote yanayotokea yanaongozwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, lakini kwa akili yake anaamini hakuna wa kumnyang'anya uongozi ndani ya chama hicho.

Mbatia alisema: "Ninaloliamini kwa utu wa kibinadamu nitalisimamia. Iwe Deni la Taifa au sekta ya elimu nitalisimamia na wala sitatereka hata ikinigharimu uhai wangu, nitasimamia kwenye ukweli na ukweli utaniweka huru."

Alidai kuwa baada ya kuona taarifa katika mitandao ya kijamii jana inayotoka katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikieleza kutomtambua kama mwenyekiti wa chama hicho, aliamua kumpigia simu Kaimu Msajili wa Vyama vya Siasa, Nyahoza, lakini hukupokea simu.

Mbatia alisema alilazimika kumpigia simu Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, ambaye alimjibu kwamba alikuwa mjini Dodoma, hivyo asubiri hadi atakaporejea Dar es Salaam leo.

"Namheshimu Msajili wa Vyama vya Siasa. Nitamsubiri hadi kesho (leo) atakaporudi ili tuzungumze na anipe ufafanuzi. Kwa sababu nilipompigia alisema hafahamu chochote kuhusu kinachotokea sasa katika chama cha NCCR-Mageuzi, " alisema Mbatia.

**MSAJILI ABARIKI**

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kubariki kusimamishwa kwa Mbatia na wenzake hao, kulitangazwa jana na Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, akisema uamuzi wa kikao cha halmashauri ya chama hicho kilichofanyika Mei 21, mwaka huu ulikuwa halali kwa akidi ya wajumbe wake. Hata hivyo, Nyahoza hakutaja uhalali wa akidi hiyo.

Nyahoza alisema kwa mamlaka ya ofisi hiyo inamtaka Mbatia kutojihusisha na siasa ndani ya chama hicho hadi uamuzi huo utakapotenguliwa na chama.

"Baada ya kusimamishwa, katibu wa chama hicho alituletea barua kwa fomu ya kisheria inayotujulisha kusimamishwa uanachama, tumekubaliana na uamuzi huo. Kama hawataridhika, ziko njia za kutafuta haki, waende mahakamani," alisema Nyahoza.

Jumamosi iliyopita, Halmashauri Kuu ya Chama cha NCCR Mageuzi ilimsimamisha Mbatia na Makamu Mwenyekiti Bara, Angelina Mtahiwa, kujihusisha na shughuli zozote za chama hadi mkutano mkuu utakapoitishwa ili wajieleze kuhusiana na tuhuma zinazowakabili.

Mbatia na wenzake walisimamishwa kutokana na tuhuma mbalimbali ikiwamo kugombanisha viongozi na hivyo kulazimika kujiuzulu.

Hata hivyo, siku moja baada ya mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama cha NCCR Mageuzi kutangaza kuwasimamisha viongozi hao, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa ya chama hicho ilikutana na kutoa maazimio manne likiwamo la kuwasimamisha nafasi za uongozi Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Ambar Hamid, Mweka Hazina, Suzan Masele na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Amer Mshindan.

Akisoma maazimio hayo, Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini la chama hicho, Mohamed Tibanyendela, alisema wamewasimamisha viongozi hao hadi pale Halmashauri Kuu itakapokutana.

Tibanyendela alisema maazimio mengine ni kutotambua mkutano wa Halmashauri Kuu uliofanyika Mei 21 kutokana na kutokuwapo kwa mujibu wa Katiba ya chama chao.

Pia alisema Kamati Kuu imelaani Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuingilia migogoro ya chama na tayari wameshamwandikia barua pamoja na mamlaka yake ya uteuzi.

Azimio lingine ni kutoitambua bodi ya wadhamini iliyoteuliwa kwa madai kuwa bodi hiyo iliyopo ni halali na inaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

Mwenyekiti wa NCCR, Mbatia, alisema chama hicho ndicho mwasisi wa mageuzi Tanzania, hivyo wanaamini katika mwafaka wa kitaifa.

# Rais Samia amkumbuka hayati Magufuli akipokea tuzo AFDB

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema tuzo ya Africa Road Builders-Babacar Ndiaye 2022, ilistahili kutunukiwa kwa Hayati Dk. John Magufuli kutokana na mchango wake mkubwa wa kusimamia maendeleo ya miundombinu nchini Tanzania.

Aliyasema hayo jana, baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo Accra nchini Ghana kama ishara ya kazi nzuri aliyoifanya ya kuboresha miundombinu nchini Tanzania, katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB), unaoendelea nchini humo.

"Heshima kubwa kusema katika jitihada zote hizo mtu mmoja alijitokeza zaidi nyakati hizi zote na huyu si mwingine zaidi ya Hayati Dk. John Pombe Magufuli, mtangulizi wangu, roho yake iendelee kupumzika kwa amani, ni bahati mbaya kwamba hayupo nasi leo kushuhudia matunda ya jitihada na uongozi wake," alisema Rais Samia kwa huzuni.

Alisema kuwa Hayati Magufuli alitumika katika uboreshaji wa miundombinu awamu ya tatu na nne za uongozi akiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na baadaye kuwa mstari wa mbele katika jitihada hizo alipokuwa Rais wa awamu ya tano.

"Nikitambua hilo ninapokea tuzo hii nikiwa bado siamini kwamba inaweza kuwa ya mtu mmoja, na kama tuzo hii ingekuwa ni ya mtu mmoja basi mtu huyo anayestahili kuliko Watanzania wote ni Dk. John Pombe Magufuli," alisema Rais Samia.

Alisema anapokea tuzo hiyo kwa hisia mchanganyiko kwa sababu utekelezaji wa miradi hiyo huchukua muda mrefu tangu upembuzi yakinifu, kutafuta pesa hadi utekelezaji na kipindi kifupi cha uongozi wake kisingeweza kutekeleza hayo yote.

Kwa Mujibu wa Rais Samia, mchakato wa ujenzi wa miundombinu ulianzia awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi hiyo chini ya Hayati Julius Nyerere, lakini jitihada zilianza kuonekana katika serikali ya awamu ya tatu chini ya uongozi wa Hayati Benjamin Mkapa, wakati ukuaji wa uchumi uliwapa uwezo wa kutoa rasilimali za ndani kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu kupitia mfuko wa barabara na misaada kutoka taasisi za kifedha kimataifa.

Alisema awamu ya nne chini ya Jakaya Kikwete, ilichukua kijiti na kufanya kazi kubwa katika kupanua mtandao wa barabara na kuhakikisha wanaunganisha maeneo mbalimbali ya nchi hiyo.

Rais Samia alisema kuwa bara la Afrika lina vigezo vyote vya kujitosheleza kiuchumi ikiwamo asilimia 60 ya ardhi inayofaa kwa kilimo, madini na maliasili za bahari, lakini vitabaki bila kutumika kama hakuna mikakati madhubuti.

"Sasa ili kusimamia vizuri rasilimali hizi Afrika, lazima izalishe, ichakate na kufanya biashara ndani ya mipaka ya bara letu ni katika muktadha huo ukanda huru wa biashara Afrika unaweza kuleta maana, ili kufikia huko miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni kigezo muhimu hasa barabara na reli," alisema.

Alisema jitihada za Tanzania kuboresha miundombinu, mradi wa kwanza ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR itaunganisha Bandari ya Hindi ya Dar es Salaam kwenda kwenye nchi ambazo hazina bahari kama Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kupitia ushoroba wa kati ambao umeshajengwa ikiwa na urefu wa kilomita 2724, huku ushoroba wa Kaskazini wa kilometa 1,028 na wa Kusini ukiwa na kilomita 1,000 ukijengwa baadaye.

Rais alisema lengo la ujenzi huo pia ni kuunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) zenye nchi sita na za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zenye nchi 16 kwa kuwa anaamini kuunganisha jumuiya za kikanda kutaunganisha bara zima.

"Bila kuwapo muunganiko wa barabara, biashara barani Afrika zitaendelea kuwa chini, kwa hiyo tukiongeza mtandao wa barabara na reli utaongeza biashara ndani ya Bara la Afrika hasa kupitia ukanda huru wa biashara huru barani Afrika."

Rais Samia aliishukuru Benki ya AFDB kwa mchango wake mkubwa katika kuisaidia nchi hiyo kuziba pengo la kugharamia miundombinu kwa kuwa ndani ya miaka 15 benki hiyo imetoa Sh. bilioni 2.93 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kadhalika alisema bado nchi inahitaji msaada kutoka kwa benki hiyo kwa kuwa kuna miradi ya miundombinu inahitaji kuboreshwa ikiwamo barabara tatu za kikanda na moja ya kitaifa ambazo ni muhimu.

**TANGAZO**

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO - MEI 2022

## Viwango unavyotozwa kwa kadri unavyotumia (Bila Kodi)

****- Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu**
**- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.1 kwa kila kilobaiti 10 za data**

**VIWANGO VYA NDANI**

| Aina za simu | Bei (Sh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 22 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 22 |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (Sh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 522 | China, India, Marekani, Canada, USA, Canada |
| Kundi 2 | 739 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 739 | Lebanon, Israeli, Hispania, U.A.E, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 869 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland, Pakistan, Yemen, Phillipines, Saudi Arabia, Netherlands, Japan, Malaysia, Norway, Ireland |
| Kundi 5 | 1304 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Oman, Ujerumani |
| Kundi 6 | 1825 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 1825 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia, Burundi, Zimbabwe, Mozambique, Switzerland, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 14342 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA SMS**

| Aina za SMS | Bei (Sh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 6 |
| SMS za kimataifa | 156 |

**DATA TARIFFS**

| Intaneti | Bei (Sh/SMS) |
|---|---|
| Data kwa MB | 7 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

**MITANDAO YOTE**

| Bei | Jumla ya Dakika | Dakika za Tigo - Tigo | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 100 | 90 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 30 | 0 | 15 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | 310 | 270 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1000 | 150 | 0 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 2000 | 220 | 70 | 30 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | 70 | 30 | 200 | 100 | Saa 24 |
| 2000 | 150 | 50 | 150 | 700 | Saa 24 |
| 1500 | 300 | 250 | 30 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 150 | 0 | 20 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 400 | 0 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | 700 | 0 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 270 | 200 | 100 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 450 | 250 | 250 | 1536 | Siku 7 |
| 10000 | 1200 | 0 | 50 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | 3000 | 0 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 30000 | 3300 | 0 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 750 | 150 | 500 | 2560 | Siku 30 |
| 20000 | 1600 | 300 | 500 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 1500 | 300 | 500 | 14336 | Siku 30 |
| 50000 | 2900 | 400 | 500 | 23552 | Siku 30 |

**KIMATAIFA**

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 30 |

**SMS**

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 500 | 0 | 500 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 5000 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

**BILA KIKOMO**

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB |
|---|---|---|---|
| 500 | 6 | 0 | 0 |
| 1000 | 30 | 0 | 0 |
| 2000 | 45 | 0 | 0 |
| 1000 | 0 | 0 | 150 |

**INTANETI**

| Bei | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 150 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 650 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 1331 | Saa 24 | N/A |
| 2500 | 1638 | Siku 3 | N/A |
| 2000 | 1024 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 1741 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 3072 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 6144 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 9728 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 5120 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 12288 | Siku 30 | N/A |
| 35000 | 22528 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 32768 | Siku 30 | N/A |

**SOCIAL & VIDEO**

| Bei | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 1000 | Youtube- Mb 650 | Saa 24 | N/A |
| 1500 | WhatsApp+Facebook+Instagram+Twitter - Mb 650 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | WhatsApp+Facebook+Instagram+Twitter - Gb 1 | Siku 7 | N/A |

**MIC TANZANIA PLC,**
Derm Complex, Kiwanja Namba 11, Kitalu 45 A, Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

tigo

216872102

# Meneja stendi Magufuli Mbezi azomewa ziara ya viongozi CCM

**Na Beatrice Shayo**

MENEJA wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi Mwisho, Dar es Salaam, Laurent Cheche, amejikuta katika wakati mgumu baada ya kuzomewa na wafanyabiashara.

Cheche alikutwa na zahama hiyo wakati akijibu tuhuma dhidi yake akidaiwa kushindwa kukiendesha kituo hicho na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Baadhi ya wafanyabiashara walitoa malalamiko yao jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, huku wakidai hawamtaki meneja huyo kwa sababu anafanya mambo tofauti na viongozi wa serikali.

Awali, Mwenyekiti wa Mawakala wa Makarani wa Mabasi Mkoani Dar es Salaam, Ephraim Wambela, alisema baadhi ya wawakilishi wa serikali wako tayari kuiangusha serikaki yao.

"Hapa kwenye kituo kuna watu wawili ambao ni meneja anaharibia Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwa sababu anatafuta miradi yake ili tumlipe mwisho wa mwezi na meneja hana uwezo wa kuendesha kituo," alisema huku wafanyabiashara wakishangilia.

Alisema meneja hayuko tayari kufanya kazi na wao na kama anataka kufanya kazi na matajiri basi apelekwe mikoani.

"Mtu mwingine ni huyu afande. Anageuza kituo cha polisi ni mradi wa madini kwa kuwakamata watu na kuwataka kulipa hela. Yaani hatufanyi biashara kwa raha," alisema Mwambale.

Malalamiko mengine yaliyotajwa ni wafanyabiashara wadogo kunyanyaswa, kuwapo na sheria za kuwaumiza, kuwapo kwa kodi kubwa, mabasi kutokushusha abiria katika kituo hicho, mgambo kuwakamata wanapokuwa wamekaa na biashara zao na vitendo vya wizi.

Baada ya kusikiliza malalamiko hayo, Shaka aliwataka viongozi hao ambao wametajwa, watoe ufafanuzi ndipo Cheche alipoema kwa mujibu wa taratibu, kodi inaanzia Sh. 40,000 na si Sh 20,000, hivyo ni vyema wafanyabiashara wakaelewa taratibu zilizopo.

Alisema ukamataji wa watu unafanyika kwa mujibu wa sheria na akilipa anapatiwa risiti na faini zao ni Sh 50,000.

"Wanaokamatwa na jiji au manispaa huwa wanalipishwa faini ya Sh 50,000 na wanapatiwa risiti kwa mujibu wa sheria," alimaliza kisha wafanyabiashara wakaanza kumzomea.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominic, alisema changamoto zote zilizojitokeza zitafanyiwa kazi. Kuhusu uwezo wa meneja, alisema wanamwona yuko vizuri kwa kuwa si taaluma yake wameomba mtaalamu kutoka TAMISEMI kusimamia kituo hicho.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, alisema atasimamia suala la ulinzi katika kituo hicho pamoja na mapato yasipotee na akaliagiza Jeshi la Polisi kuchukua hatua kwa waliotajwa kufanya unyanyasaji dhidi ya wafanyabiashara kituoni hapo.

Shaka alisema chama kina wajibu wa kufuatilia na kutathmini na kuona kazi wanayoifanya na serikali waliyoiweka madarakani na jana wametekeleza matakwa ya ilani ya CCM.

Alisema kuna vitendo vya rushwa wameona namna gani askari mgambo wamejitengenezea vianzio vya mapato katika eneo la Feri.

"Pale Feri askari mgambo wamejitengenezea mapato ambayo sio rasmi ndio maana nikasema kabla ya kufika hapa nilifanya ziara peke yangu nilitaka kujifunza wale wafanyabiashara wa jioni hata hana kosa la kisheria ambalo anatakiwa kuwajibika basi wao mgambo wanajitengenezea sheria za kwao wengine wanadai faini kati ya Sh. 50,000 hadi 150,000 na wakati mwingine wanachukua bidhaa za wanyonge chama tumeliona hilo," alisema Shaka.

Shaka alisema malalamiko ni mengi katika soko la Feri na kutoa siku saba kwa viongozi na wananchi wa soko hilo kukutana kwa pamoja na kuangalia namna ya kutatua matatizo yao.




Mkuu wa Kituo cha Polisi Chang'ombe, SSP Ariziki Makwaya, akizungumza kwenye mkutano wa kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto (MTAKUWWA), Mkoa wa Dar es Salaam jana, uliokuwa ukijadili mikakati ya kutokomeza vitendo vya ukatili katika jamii. Kushoto ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Baba na mwana wahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Musoma kupitia Mahakama ya Wilaya Tarime, mkoani Mara, imewahukumu baba na mtoto wake wa Kijiji cha Genkuru, kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya mauaji.

Waliohukumiwa ni Matinde Keranganyi (baba) na Mwita Matinde (mtoto), ambao walishtakiwa kwa kumpiga mawe, kumkata mapanga na kumchoma mkuki Chacha Nyamhanga, wakigombea ardhi.

Hukumu hiyo ilisomwa na Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, Frank Moshi.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Yese Temba, alidai kuwa washtakiwa Mei 25, 2019 kwa makusudi wakiwa na

silaha za jadi walimvamia Nyamhanga akiwa shambani kwake kumshambulia kwa kumpiga mawe na kuanguka chini na kisha kumchoma mkuki na kumkata mapanga kichwani hali iliyosababisha kifo chake.

Chanzo cha mauaji hayo kimedaiwa kuwa ni mgogoro wa ardhi kati ya marehemu na washtakiwa hao.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Mwanasheria wa Serikali Temba ulileta mashahidi saba vikiwamo vielelezo na PF3, mganga aliyefanya uchunguzi wa mwili wa marehemu na upande wa utetezi ulileta mashahidi wanne.

Msajili wa Mhakama Kuu, Moshi alisema mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila kuwapo shaka lolote.

# Spika: Marufuku sarakasi na kupiga magoti bungeni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema hairuhusiwi mbunge kuchangia bungeni akiwa amepiga magoti au kupiga sarakasi.

Alitoa kauli hiyo juzi baada ya Mbunge wa Igalula, Venant Protas, kuomba mwongozo wa Spika, akitaka kufahamishwa kama kanuni za Bunge zinaruhusu mbunge kuchangia akiwa amepiga magoti au kupiga sarakasi.

"Hili haliruhusiwi ukiwa unachangia au ukiwa unafanya kitu chochote humu ndani, labda wale wanaopiga magoti kwa maana yule anayezungumza naye anaona itakuwa siyo heshima au anataka alingane naye kwa sababu amekaa, lakini kwa maana ya uchangiaji, unasimama mahali pako unawasha kisemeo, unasema hoja zako zitasikika bila kufanya kituko chochote.

"Kwa sababu hili limeombwa kwa leo (juzi), niseme hairuhusiwi, vivyo hivyo hairuhusiwi kupiga sarakasi humu ndani, kwa mukhtadha huo, asije mwingine akafanya jambo ambalo linaashiria kwamba anachangia kwa namna ambayo nimeshatoa hapa maelekezo, huyo atakuwa anataka tuchukue hatua nyingine na tutafanya hivyo," alionya.

Alisema watafanya hivyo kwa sababu wamejiwekea kanuni na jumba hilo (Bunge) ni rasmi na hivyo wabunge lazima wawe rasmi.

"Ndiyo maana tunaitwa waheshimiwa wabunge. Kuna jambo lingine ninakumbushwa hapa, 'na kulia je?' Waheshimiwa wabunge, kuhusu kulia, kulia ni hisia labda kama mtu atakuwa amefanya cha ziada katika kulia kwake lakini kulia ni hisia, ni tofauti na haya mengine ambayo yanaashiria kufanya jambo la ziada, ambayo kimsingi hayo mambo humu ndani ni marufuku," alifafanua.

Mbunge Protas alitumia kanuni ya 16 kuomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge huku akieleza kuwa kumeibuka jambo wakati wabunge wanapopata kuchangia au kupeleka kero za wananchi wanapitia utaratibu wa kujiorodhesha na kiti kinatoa nafasi ya kusema kero.

"Mwongozo huu mbunge anapopewa nafasi lazima achangie akiwa kasimama lakini sasa kumeibuka baadhi ya wabunge wanachangia wanavyojua wenyewe, achana na jana, leo mheshimiwa mmoja amechanga kwa kupiga magoti. Je, katika mwongozo huu Kanuni za Bunge, hii ni sawa?"

Alihoji mbunge huyo.

**HABARI KITAIFA**

# Makusanyo uvuvi yaporomoka, mbunge asema sekta iko hoi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAKATI Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akitaja sababu kupungua kwa makusanyo ya maduhuli katika sekta ya uvuvi, Mbunge wa Viti Maalum CCM, Mariam Ditopile, amesema viwanda vinafanya kazi kwa siku nne badala ya saba kwa wiki.

Akiwasilisha jana bungeni makadirio ya mapato na matumuzi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri Ndaki alisema makusanyo ya 2021/22 wizara ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 40 lakini hadi Aprili 30, mwaka huu, Sh. bilioni 19.171 zilikusanywa sawa na asilimia 63.9 ya lengo.

Waziri Ndaki alitaja miongoni mwa sababu za kutofikia lengo la makusanyo ni uwapo wa mianya ya utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenye maeneo ya maji na mipakani.

"Kuwapo kwa wavuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi; upungufu wa watumishi sekta ya uvuvi kwenye vituo vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi na uthibiti ubora wa viwango wa masoko, ufinyu wa bajeti na uhaba wa vitendea kazi kwenye baadhi ya vituo kama magari, pikipiki, na boti, kuwapo kwa ukwepaji wa ulipaji wa ushuru kwa mazao yanayosafirishwa nje," alisema.

Alisema fedha hizo zimekusanywa kupitia leseni za kusafirisha samaki na mauzo yake, za uingizaji mazao ya uvuvi, ushuru wa mrahaba, leseni za uvuvi ukanda wa uchumi wa bahari kuu, tozo za maabara, leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini za ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

Akichangia bajeti hiyo mbunge Ditopile alisema hali ya upatikanaji wa samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria ni mbaya na hafahamu kama kwenye vipaumbele vya wizara hiyo wameliona hilo.

"Kwa nini ninasema hali mbaya? Sangara ni bidhaa katika soko la samaki la duniani, Ulaya ndiyo soko kubwa ambalo zaidi ya asilimia 70 ya mazao ya samaki yanayotoka Afrika yanakwenda huko. Mwaka 2014/15 Tanzania tulikuwa tunatoa tani zaidi ya 45,000 za minofu ya sangara na mazao yake lakini mwaka 2021 tumetoa tani 14,000 tu lakini viwanda vyetu vimekuwapo mwaka 2014/15 tulikuwa tunaajiri zaidi ya vijana 12,000 kwenye sekta hii.

"Ninasikitika kusema ajira zimepungua zaidi ya asilimia 50 na leo hii tuna takribani vijana 4,000 tu ambao wameajiriwa kwenye sekta hii, leo hii wabunge wa mikoa ya Mwanza na jirani ni mashahidi, ukienda kuhoji machinga waliopo mtaani, miaka 10 nyuma wengi walikuwa waajiriwa wa viwanda hivi lakini hapo zamani viwanda vilikuwa vinafanya kwa shift (awamu) tatu," alisema.

Mbunge huyo alisema viwanda hivyo vilikuwa vinafanya kazi wiki nzima lakini hali ya sasa vinafanya kazi kwa zamu moja na nusu kwa siku na siku nne kwenye wiki.

Alisema ametoa picha hiyo ili wafahamu royalty iliyokuwa inapatikana kwenye sangara ilisaidia kujenga hospitali, vituo vya afya na maeneo mengine ndani ya nchi.

"Nimeangalia hotuba ya mheshimiwa waziri bado sijaona je, na ninaamini jambo linalosababisha hali hii ni uvuvi haramu lakini nimesikitika kuona katika vipaumbele vya wizara sijaona palipoandikwa mna mkakati wa aina gani madhubuti wa kupambana na uvuvi haramu.

"Nimefuatilia je, mheshimiwa waziri unazo takwimu za viwanda ulivyonavyo kwa sababu kati ya wageni mliowaalika kuja kuhudhuria bungeni, wamiliki wa viwanda mmealika prime catch lakini imefungwa miaka 10 iliyopita hakipo, kuna kiwanda kinaitwa King Fish hakipo kilishafungwa," alisema.

Alisema leo hii Uganda ambayo ina sehemu ndogo ya Ziwa Victoria inawaongoza kwa kuwa na idadi ya viwanda vingi kuliko Tanzania na katika nchi za Afrika zinazopeleka minofu soko la dunia nchi hii haipo lakini Uganda ni ya 10 barani humo.

"Ninaongea kwa masikitiko makubwa yapo maeneo ambayo Mungu ametubariki mno, kikubwa ni utashi wa kutambua tatizo lipo wapi tukapata udhubutu wa kushughulikia tatizo hili ili kunusuru haya, huko nyuma kuna operesheni ilianzishwa kwa ajili ya uvuvi haramu almaarufu 'operesheni sangara' nia ilikuwa njema lakini niulize kama wizara je mnayo tathmini ya operesheni kwa sababu kwa wananchi leo ukiwauliza kuhusu operesheni hii ni majeraha matupu," alisisitiza.

Alisema ni operesheni iliyokw-Pia alisema dagaa wanaopatikana Ziwa Tanganyika ni nzuri lakini mpaka leo biashara zake ni kiholela ambapo Rukwa, Katavi hakuna kiwanda kikubwa cha samaki.

"Ukiacha dagaa kuna samaki wazuri tuna migebuka wanaita kuku wa ziwani serikali imejipangajie kuvutia uwekezaji wa kiwanda kikubwa ziwa Tanganyika, kama hamna taarifa ninayo wapo wawekezaji wanataka kuweka kiwanda, tangu waanze mchakato umekuwa mchakato, fuatilieni mjue," alisema.

Pia alisema walikuwa na mpango wa kuanzisha viwanda ukanda wa bahari miaka sita iliyopita na kuhoji kipindi chote cha kujinasibu na Tanzania ya viwanda kuna kiwanda kipya kimeanzishwa na kama bado sababu ni zipi.

"Kilimo tulikuwa tunapiga kelele iongezewe bajeti miaka yote lakini imeongezeka, wizara hii mmeniangusha wizara hii haijanigusa naomba kama mnamajibu ya matumaini mapya mje nayo wakati mnahitimisha mjadala," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwamtumu Zodo, alisema cha kusikitisha mikakati ya mwaka 2021/22 waliyokuja nayo wizara hakuna hata mmoja waliotekeleza.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Mashimba Ndaki, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chongolo ataja mwarobaini wa utatuzi wa ajira Afrika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka wanafunzi wanaoshiriki mafunzo katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, kushirikiana na viongozi wa vyama na serikali kutumia nguvu kazi hasa vijana kutatua tatizo la ajira.

Amesema njia pekee inayofaa katika kutatua tatizo hilo ni uzalishaji katika sekta mbalimbali.

Chongolo aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo kwa makada 120 vijana wa vyama sita vya ukombozi kusini mwa Afrika yanayofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kwa Mfipa, Kibaha.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza tatizo la ajira kwenye nchi zao, tatizo ambalo linakuwa kubwa kwa sasa.

Kwa mujibu wa Chongolo, vijana wanatakiwa kutumia vizuri mafunzo wanayoyapata katika shule hiyo ili kujenga ujamaa katika masuala ya msingi ya uongozi kwa nyakati za sasa kwenye vyama vyao kulingana na wakati uliopo.

Alisema kufunguliwa kwa shule hiyo, kumetoa nafasi nzuri kwa makada wa vyama hivyo hasa kwa vijana kwa kuzingatia mabadiliko ya wakati na nyakati yatakayosaidia kuendesha vyama vyao kwa maslahi ya wananchi.

Chongolo alisema mafunzo hayo ya awamu ya tatu ambayo ni maalumu kwa makada vijana, yatajikita katika uongozi kwenye masuala ya maslahi, itikadi na misingi ya ujamaa.

Alisema makada hao vijana pia watajifunza namna vyombo vya uamuzi kwenye vyama vyao na serikali vina nguvu kiasi gani na vinafanyaje kazi katika kuisaidia serikali kufikia yale ambayo wananchi wana kiu nayo.

"Muhimu kwa makada ni vyema kujua vyombo vya uamuzi kwenye vyama vyao na kero za wananchi na namna ya kuyashughulikia kulingana na mabadiliko yaliyopo sasa," alisema Chongolo.

Alisema vyama hivyo vimetoa nafasi kwa makada hasa wa kizazi cha sasa kukaa pamoja kujifunza masuala ya uongozi kwa kuzingatia mabadiliko ya wakati na nyakati na yatakayosababisha kuboresha vyama vyao.

Chongolo alikishukuru Chama cha Kikomunisti cha China kinachotawala nchi hiyo kwa kusaidia kufanikisha mafunzo hayo. Alisema nchi hiyo imekuwa rafiki wa Tanzania kwa muda mrefu na kusaidia katika mambo mbalimbali ya kimaendeleo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali Ngemela Lubinga, alisema kabla ya kuanzishwa kwa shule hiyo hapakuwa na sehemu ya kuandaa vijana kuwajenga kistadi kwa kuwa tayari na mabadiliko.

Alisema kwa sasa dunia inaenda kwa kasi hivyo ni lazima viongozi waandaliwe na kazi inayofanywa kwa sasa ni kutengeneza viongozi wa nchi wanaoendana na mabadiliko yaliyopo.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo kutoka Mkoa wa Pwani, Hadija Ismail, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuwaandaa makada vijana kuendana na mabadiliko yaliyopo kwa sasa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU**
**WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI**

OSHA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) unapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa unatarajia kuuza mali zake chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara katika Ofisi zake zilizopo Barabara ya Mahakama, Kinondoni karibu na Shule ya Sekondari Kambangwa siku ya Jumamosi tarehe **04/06/2022** kuanzia saa nne **(4:00)** asubuhi. Zifuatazo ni mali zinazokusudiwa kuuzwa÷

1) Magari manne (4) aina ya Suzuki Jimmy.
2) Jenereta.
3) Vifaa mbali mbali vya TEHAMA.

**MASHARTI YA MNADA**

(i) Gari/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo (as is where basis)

(ii) Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari atakalonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi nan ne (14) kuanzia siku ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atapoteza haki zote za ununuzi wa gari husika na amana iliyolipwa haitarudishwa.

(iii) Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (Value Added Tax) hivyo mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi kabla ya kuchukua gari kutoka eneo la Ofisi za OSHA.

(iv) Kwa upande wa vifaa vinginevyo, mnunuzi atalipa asilimia mia moja (100%) ya thamani ya kifaa/vifaa atakavyonunua na kuchukua kifaa/vifaa atakavyokuwa amenunua siku ya mnada.

(v) Ruhusa ya kuangalia mali zinazokusudiwa kuuzwa itatolewa siku (2) kabla ya tarehe ya mnada.

Imetolewa na:
**MTENDAJI MKUU**
**WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)**
**S.L.P 519, DAR ES SALAAM**
**Simu Bila Malipo: 0800110091/2, Barua Pepe: info@osha.go.tz,**
**Tovuti: www.osha.go.tz**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuzo ya Rais Samia chachu kuwa na miundombinu bora

**RAIS** Samia Suluhu Hassan jana alipokea tuzo ya Africa Road Builders-Babacar Ndiaye 2022 ambayo Tanzania imepata kutokana na maendeleo ya miundombinu ambayo ndicho kichocheo kikubwa kwa maendeleo ya uchumi na ya kijamii katika taifa lolote.

Pamoja na kwamba Rais Samia alipokea tuzo hiyo, aliweka bayana kuwa angestahili kutunukiwa Hayati Dk. John Magufuli, mtangulizi wake, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa kuanzia mwaka 2016 hadi sasa. Katika hilo, Rais ameonyesha uungwana mkubwa kupongeza kazi ya mtangulizi wake.

Kushinda kwa tuzo hiyo ambayo hutolewa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kwa nchi iliyofanya vizuri katika uendelezaji wa miundombinu, kunaonyesha dhahiri kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa katika sekta hiyo.

AfDB kila mwaka imekuwa ikitoa fedha za mikopo ya masharti nafuu kwa nchi za Afrika kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu na Tanzania imekuwa mnufaika mkubwa wa benki hiyo kutokana na kila mwaka kupokea mabilioni ya shilingi kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu.

Kwa hakika, katika serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli na ya sasa chini ya Rais Samia, kumekuwa na maendeleo makubwa ya ujenzi wa miundombinu kama vile barabara na reli ikiwamo reli ya kisasa (SGR) na viwanja vya ndege sambamba na ununuzi wa mabehewa ya treni.

Katika ujenzi wa barabara, kumekuwa na kazi kubwa kuhakikisha barabara nyingi zinazounganisha mikoa na baadhi za wilaya, hususan zile za kimkakati, zinajengwa kwa kiwango cha lami chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na zingine zikijengwa kwa changarawe ili zipitike kipindi chote cha mwaka zikiwa zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Jijini Dar es Salaam, kwa mfano, barabara nyingi zinajengwa pamoja na madaraja ya juu sambamba na kupanua zingine ili kupunguza msongamano wa magari na kuwezesha watu kuwahi katika shughuli zao za uzalishaji na kurejea nyumbani kwa wakati. Pia katika reli imeshuhudiwa ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ukiwa katika hatua nzuri huku vipande vya kutoka Morogoro hadi Makutopora na baadaye kufika Mwanza hadi Kigoma kazi ikiwa inaendelea.

Hiyo ni mifano michache ya kazi kubwa inayoendelea kwa sasa na katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha, matrilioni ya shilingi yametengwa ili kutekeleza azma hiyo ya ubora wa miundombinu.

Kwa ujumla, tuzo hiyo inapaswa kuwa kichocheo kikubwa katika uendelezaji wa kazi iliyoanzishwa ili Tanzania iwe na miundombinu bora ya usafirishaji kwa ajili ya wananchi na bidhaa mbalimbali kutoka zinakozalishwa hadi sokoni.

Kukamilika kwa miundombinu hiyo pia kutapunguza kama si kuondoa kabisa kero ya wananchi hasa waishio maeneo ya vijijini ambao nyakati za masika wamekuwa wakipata matatizo ya usafiri kutokana na ubovu wa barabara. Sambamba na kushindwa kusafirisha mazao yao yamekuwa yakiozea mashambani.

Aidha, sifa hiyo njema ya Tanzania kimataifa hadi kupata tuzo hiyo, isiharibiwe na baadhi ya watendaji wa serikali kwa kushindwa kusimamia kazi ili ziwe na ubora kwa kuendekeza rushwa kutoka kwa makandarasi au kuwaachia makandarasi wafanye kazi kwa kulipua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Nimeipenda kampeni ya Kipunguni Dar, 'Jihadhari na Kamba ya Kisima'

Na Sabato Kasika

**KWA** ubunifu huu wa kulinda afya, huenda ukasaidia kuleta matokeo, kwa kuwasaidia wananchi kuepuka magonjwa mbalimbali yakiwamo ya mlipuko kama kipindupindu na mengine.

Ni ubunifu gani huo? Ni kwamba, Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na wadau wa afya wa Kata ya Kipunguni imeanzisha kampeni iitwayo 'Jihadhari na Kamba ya Kisima.'

Kampeni hiyo inahusu utaratibu wa kuweka ndoo ya maji tiririka, sabuni na vitakasa mikono pembeni mwa visima vya maji vinavyomilikiwa na watu binafsi katika kata hiyo, ili kila anayefika kuteka maji anawe kwanza.

Ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipinguni, Seleman Bishagazi ni kwamba wananchi wanateka maji kwa kutumia kamba iliyofungwa kwenye chombo cha kutekea.

Kwa kuwa kamba inayotumika ni moja kwa kila kisima na inashikwa na watu wote kwa nyakati tofauti, inaweza kuwa rahisi kwao kukumbwa na magonjwa ya mlipuko, iwapo mmoja wao atakuwa amenaswa na maambukizi.

Hivyo kwa hali hiyo, kituo cha kushirikiana na wadau wa afya kikabuni utaratibu huo wa kuweka huduma hiyo pembeni kwa kisima, ili kila anayetaka kushika kamba achote maji, lazima anawe kwanza kujihakikishia usafi.

Mkurugenzi huyo anasema katika kampeni hiyo, kwamba zaidi ya ndoo 60 zimeshawekwa pembeni mwa visima vya maji ndani ya Kata ya Kipunguni, ambazo zimenunuliwa na wadau wa afya.

Binafsi ninaona kampeni hiyo inaweza kuwa na manufaa kutokana na kwamba katika maisha haya, kila mtu ana njia yake ya kuzingatia usafi na wapo wengine hawazingatii.

> **Nitoe mfano, mtu anaweza kwenda kujisaidia na kuondoka bila kunawa mikono kwa kutumia sabuni, hivyo akishika kamba ya kutekea maji, anaweza kuacha vijidudu na kuambukiza wengine magonjwa ya mlipuko na ndio mwanzo wa kisambaa kwake.**

Nitoe mfano, mtu anaweza kwenda kujisaidia na kuondoka bila kunawa mikono kwa kutumia sabuni, hivyo akishika kamba ya kutekea maji, anaweza kuacha vijidudu na kuambukiza wengine magonjwa ya mlipuko na ndio mwanzo wa kisambaa kwake.

Hivyo, ninadhani ubunifu kama huu, unafaa kuigwa na watu wa maeneo mengine ambayo wakazi wake wanatumia maji ya visima, ili kulinda afya zao na za wengine badala ya kuendelea kufanya kienyeji.

Nikumbushe tena kuwa mtu anaweza kutoka nyumbani ikiwa na maambukizi na kushika kamba na kuwaachia wengine maradhi. Hapo ndio inatushinikiza katika haja ya kunawa kwa maji tiririka. Kutokana na mazingira hayo, ubunifu huo unakuwa muhimu, hivyo si vibaya hata wamiliki wa visima wenyewe wakabeba jukumu hilo wa kuweka ndoo za maji tiririka pembeni mwa visima vyao.

Suala la hamasa kwa jamii kuwa na ubunifu unaosaidia kulinda afya ni muhimu, ili kuhakikisha jamii inapata uelewa wa kutosha kuhusu mbinu za kuepuka magonjwa mbalimbali yakiwamo ya mlipuko.

Wakati wote na kila sehemu, afya ni msingi wa maendeleo na mara zote bila ya kuwa na afya njema, mtu hawezi kufanya shughuli yoyote ya kujiletea maendeleo. Hivyo, suala la kubuni mbinu mbalimbali za kulinda afya ndani ya jamii ninaamini ni jambo linalotakiwa kuwekewa mkazo, huku Kipunguni nako kunafaa kuwa darasa la kujifunza kwa wahitaji walioanza na wasioanza kupata huduma ya aina hiyo kwingineko.

# Mbaroni tuhuma utapeli wa kuuza viwanja

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashilikia watu 48 kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo utapeli kuuza kiwanja zaidi ya mara moja na uporaji kwa kutumia bodaboda.

Pia wamo wacheza karata za kamari.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Muslim, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwa nyakati tofauti baada ya operesheni maalumu iliyoendeshwa mjini hapa kudhibiti matukio hayo.

Kuhusu wanaotuhumiwa kuhusika na utapeli wa viwanja alisema, watuhumiwa 16 wamekamatwa kwa kughushi nyaraka kugonga mihuri bandia na kuuza maeneo mbalimbali yasiyokuwa ya kwao katika Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na watu wengine kutoka nje ya mkoa huo.

"Wamekuwa wakiandaa mihutasari feki na hati bandia za umiliki na uuzaji wa ardhi na kuuza maeneo hayo kwa watu wakishirikiana na baadhi ya watendaji wa taasisi, mamlaka na idara mbalimbali za serikali katika kufanya uhalifu na kuwa kero, kuzua taharuki katika jamii hata kutishia uvunjifu wa amani," alisema Musilim.

Watuhumiwa hao ni pamoja na mfanyabiashara maarufu wa mjini Morogoro Mustakhim Abdulsadick (33), mkazi wa Forest, Zebio Ngunga (40), mkazi wa Mazimbu, Zena Shomari, mkazi wa Kiwanja cha Ndege, Hussein Said Ally (44), mkazi wa Mazimbu na Athumani Masala, Patrick Lesimo, Joseph Mayani (56) na Deogratius Nyami (40) wakazi wa Mkundi.

Wengine ni Mwenyekiti wa CCM, Area six, Karazi Anthony Karamagi, Yohana Ntawa (38), mkazi wa Kiegea B, Zakaria Msamaka (44), mkazi wa Kihonda, Metusela Yusuph (48), mkazi wa Dar es Salaam na Nyamizi Athuman, mkazi wa Mawenzi, Joyce Ndonde, mkazi wa maghorofa ya Kilakala.

Kamanda alisema polisi wanaendelea kuwasaka watuhumiwa wengine waliotoroka ama kuhama mkoa wanaotuhumiwa kujihusisha na matukio hayo ya utapeli wa viwanja na kuwataka kujisalimisha kwa hiyari.

Katika tukio jingine Kamanda Musilim alisema wamewatia mbaroni vijana 25 wenye umri kati ya miaka 16 hadi 21 wakituhumiwa kujihusisha na uchezaji wa karata za kamari katika mapagale na nyumba mbovu nyakati za usiku.

Tukio jingine limehusisha kukamatwa kwa wapanda bodaboda saba, maarufu kama Vishandu wakidaiwa kujihusisha na wizi wa simu na pochi kwenye maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro.

Kamanda Muslim alisema wapanda bodaboda hao wamekamatwa maeneo ya Msamvu mzunguko, stendi ya Dodoma, Ipoipo, Mkundi, Chamwino, Nanenane, Modeko, Kihonda na Masika.

Pia kamanda alisema watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa na polisi na baada ya kukamilika watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.




## Sirro ataka elimu kukomesha mauaji ya imani za kishirikina

**Na Neema Hussein,**
MPANDA



MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amelitaka jeshi hilo mkoani Katavi kuweka mkazo katika kutoa elimu kuhusu mauaji yanayoendelea ndani ya mkoa yanayohusiana na imani za kishirikina.

IGP Sirro ameyasema hayo jana baada ya kuzindua zahanati ya polisi mkoani Katavi na kusema hali ya kiusalama katika mkoa iko vizuri isipokuwa mauaji yanayotokana na imani za kishirikina.

Alisema zahanati aliyoizindua imegharimu zaidi ya Sh. milioni 100 sambamba na kuwataka madaktari kutoa huduma bora kwa wagonjwa na kuficha siri zao.

"Lazima waheshimu wateja, lazima wajali wateja, lazima wafiche siri za wateja na kuhakikisha gharama wanazolipa wateja au wagonjwa zinaendana na uhalisia lakini kikubwa wa matumizi ya fedha za zahanati yawe wazi," alisema.

Sambamba na hilo, IGP Sirro aliwataka wanasiasa kufuata sheria katika siasa zao na kwa yeyote atakayekiuka, hatosita kumchukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusufu, ambaye alimwakilisha mkuu wa mkoa wa Katavi katika uzinduzi huo, alisema uwapo wa zahanati hiyo utasaidia kupanua wigo wa matibabu kwa wananchi.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema watahakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi na kwamba zahanati hiyo ipo kwa ajili ya watu wote na si polisi pekee.

Akisoma taarifa fupi, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Omary Seleman, alitaja changamoto zinazoikabili zahanati hiyo kuwa ni pamoja na ukosefu wa gari la wagonjwa.

# Kasi ujauzito wanafunzi yamnyima usingizi DC

**Na Happy Severine,** BUSEGA

MKUU wa Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, Gabriel Zacharia, amesema kasi ya wanafunzi wa kike kupewa ujauzito katika wilaya yake inazidi kuongezeka jambo ambalo linamnyima usingizi.

Zacharia alisema hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichofanyika mjini Nyashimo.

Alisema kila mwezi kwenye kikao cha kamati ya ulinzi na usalama wilayani hapa, matukio ya wanafunzi kupewa mimba yamekuwa yakionyesha yanaongezeka.

"Matukio mengi ambayo tumekuwa tukikutana nayo kwenye kamati ya ulinzi na usalama kila mwezi. Mengi ni mimba kwa wanafunzi wa kike na tatizo hili limekuwa kubwa sana. Kila tunapokaa kikao matukio mengi yanayokuwepo ni mimba za wanafunzi," alisema Zacharia.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kati ya mambo ambayo yamekuwa yakisumbua ni matukio hayo ya wanafunzi wa kike kupewa ujauzito na vijana.

" Tatizo hili ni moja kati ya vitu ambavyo leo ukiniuliza kitu gani kinachokusumbua akili nitasema ni mambo ya mimba," alisema.

Katika kikao hicho, mkuu huyo wa wilaya aliwataka madiwani kushirikiana na serikali katika kupambana na tatizo hilo huku akiwataka kwenda kuwaelimisha wananchi kuacha kuharibu ushahidi pindi wahusika wanapofikishwa mahakamani.

"Kinachofanya mambo haya yawe magumu ni huu utaratibu ambao wahusika humalizana kifamilia, hivyo kusababisha mwanafunzi aliyepewa ujauzito kuharibu ushahidi. Tusaidiane kupambana na tatizo hili," alisisitiza.




Mkurugenzi wa Udhibiti, Ufuatiliaji na Tathimini wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Jofrey Oleke (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuanza mwaka wa masomo 2022 /2023. Kulia ni Mkurugenzi wa Upimaji Mitaala na Ufuatiliaji wa baraza hilo, Dk. Annastella Sigwejo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Jela miaka 30 kunajisi mtoto

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Iringa, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela, Geoffrey Mtokama (21) mkazi wa Kijiji cha Igluba wilayani Iringa, baada ya kupatikana na hatia ya kumnajisi mtoto wa kike wa miaka tisa.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri umepinga adhabu hiyo kuwa ni ndogo kulinganisha na ukubwa wa kosa lenyewe.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Emmy Nsangalufu alisema Mtokama anahukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kumnajisi mtoto huyo.

Akisoma maelezo mbele ya hakimu huyo, mwendesha mashtaka Alice Thomas akisaidiana na Jacqueline Nungu, alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa Juni 13, 2021 katika kijiji cha Igluba wilayani Iringa, Mkoa wa Iringa.

Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka, mtuhumiwa huyo ambaye ni mchunga ng'ombe, alikwenda nyumbani kwa mtoto huyo usiku baada ya kugundua wazazi wake walikuwa kwenye sherehe ya pombe kijijini hapo na kumrubuni kwamba anaitwa na mama yake.

Thomas alidai kuwa baada ya kufanikiwa kumdanganya, alimpeleka sehemu na kumnajisi kisha kumsababishia maumivu sehemu za siri na kutokomea porini.

Baada ya wazazi wa mtoto kurudi toka kwenye sherehe, alidai kuwa mtoto huyo alimwambia mama kilichotokea na alipomchunguza sehemu zake za siri alikuta damu zinatoka.

Alidai kuwa baada ya hapo, shughuli ya kumsaka kijana huyo ilianza usiku wa manane na kufanikiwa kumkuta akiwa amejificha kichakani karibu na pori la kijiji, hivyo kumpeleka katika serikali ya kijiji na hatimaye polisi na kesi ikafunguliwa.

# Watakiwa kudhibiti sumu kwenye mazao

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

WAFANYABIASHARA, wasafirishaji na wasindikaji wa mazao ya mahindi, karanga na bidhaa zake wametakiwa kutumia elimu wanayopewa kudhibiti sumukuvu kwenye mazao yao ili yakubalike sokoni.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Bahi mkoani Dodoma na Ofisa Viwango wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Ally Kingazi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti kuhusu mafunzo hayo yanayoendeshwa na shirika hilo kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC).

Alisema wametilia mkazo mafunzo hayo kutokana na tathmini ya tatizo la sumukuvu ambayo ilifanyika katika wilaya 18 Tanzania Bara, ambapo taarifa ya tathmini hiyo ilionyesha kuna uelewa mdogo juu ya tatizo la sumukuvu kwa wadau hao na hivyo tathmini hiyo ilipelekea kutilia mkazo elimu hiyo.

Tatizo la sumukuvu, alisema lina athari nyingi ikiwamo kudhohofisha biashara kwa sababu mazao ambayo yamechafuliwa na sumukuvu yakigundulika ina maana hayawezi kuingia sokoni badala yake yatalazimika kuteketezwa.

"Kwa hiyo sumukuvu inachangia kudhohofisha biashara na kushusha uchumi," alisema Kingazi na kuongeza kwamba sumukuvu ina athari za kiafya kwa sababu imekuwa kisababishi cha saratani ya ini, koo na saratani nyingine.

Alifafanua kwamba wametilia mkazo elimu hiyo kwa ajili ya kuilinda jamii na walaji wanaotumia chakula kinachotokana na mazao hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yanachafuliwa na sumukuvu.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, akifungua mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo ni muhimu, hivyo aliishauri TBS kuhakikisha utaratibu huo unakuwa endelevu.

Alisema anatambua nafasi ya wafanyabiashara, wasindikaji na wasafirishaji kwa ujumla katika kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu kwenye mazao, ndiyo maana TBS imeandaa mafunzo haya mahususi kwa ajili ya kuwajengea uwezo juu ya udhibiti wa sumukuvu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma, Dk. Hamis Kanachi, alisema usalama wa chakula unatakiwa kupewa kipaumbele ili kulinda afya ya jamii na uchumi wa nchi kwa sababu ndicho kigezo muhimu katika biashara ya kitaifa na kimataifa.

Alifafanua kuwa chakula kisicho salama husababisha madhara ya kiafya na hata vifo kwa walaji pamoja na kusababisha athari za kiuchumi.

Dk. Kunachi, alisema kwa sasa usalama wa chakula unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa sumukuvu ambayo husababisha madhara ya kiafya na hata kiuchumi.

Aliwataka washiriki hao watakaporejea kwenye shughuli zao kuyatumia katika udhibiti wa sumukuvu.

"Ni matumaini yangu kuwa kwa kufanya hivyo mafunzo yetu yatakuwa yamekidhi matarajio yaliyokusudiwa kwa washiriki na wakufunzi kwa upande mwingine," alisema Dk. Kunachi.

"Kwa sababu hiyo, sisi sote tunapaswa kuzingatia mikakati ya kukabiliana na changamoto ya sumukuvu ili vyakula vyetu viendelee kuwa salama kwa muda wote," alisema.

# Jaji Mkuu wa Uganda atembelea mahakama

**Na Grace Gurisha**

JAJI Mkuu wa Uganda, Alfonse Chigamoy Owiny-Dollo, ametembelea Mahakama ya Tanzania akiambatana na maofisa 12 kwa lengo la kubadilishana uzoefu na viongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

Jaji Owiny-Dollo, aliwasili juzi mkoani Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, ambayo yalilenga kujenga ushirikiano katika masuala mbalimbali yanayohusu vyuo vya Mahakama na atakuwapo nchini kwa ziara ya siku tatu.

Alisema wamekuja nchini kupata maarifa na wanatumai kujifunza mengi kutoka katika chuo hicho na pia kupata uelewa jinsi ya kuijengea uwezo wa Taasisi ya Mafunzo ya kimahakama ya nchini Uganda.

Kwa upande wake, Profesa Juma alisema, anashukuru kwa ugeni huo kwa kuja hapa nchini, kwa sababu wamekuwa wakikutana majaji wakuu katika mikutano yao mbalimbali, lakini hajawahi kukutana kwenye vyuo vyao vya sheria na kubadilishana uzoefu.

Alisema mwezi uliopita walikuwa nchini Zimbabwe (majaji wakuu) kuzungumzia masuala ya matumizi ya teknolojia na wanadhani hilo eneo jipya wanalotakiwa kwenda nalo.

Profesa Juma, alisema ameagiza chuo hicho kuandaa kozi za kuwajengea uwezo maofisa wa Mahakama ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

"Nimekiomba chuo chetu kuangalia jinsi tunavyoweza kwenda kidijitali ili watusaidie katika eneo hili, mambo mengi tutakwenda kujifunza tukifika Lushoto," alisema.

Kuhusu ziara hiyo, Jaji Juma alisema wageni hao watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya chuo na vivutio mbalimbali vilivyoko katika Wilaya ya Lushoto.

Alisema wageni hao watapata fursa ya kubadilishana uzoefu na viongozi wa chuo hicho wa namna vinavyofanya kazi. Ziara hiyo ni sehemu ya ushirikiano kati ya Mahakama ya Tanzania na Mahakama ya Uganda na ujirani mwema kati ya nchi hizo mbili.

**Profesa Juma, alisema ameagiza chuo hicho kuandaa kozi za kuwajengea uwezo maofisa wa Mahakama ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.**

# Upelelezi kesi mawakili madai kughushi nyaraka wakamilika

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kughushi nyaraka za nguvu ya kisheria inayomkabili raia wa Ufaransa na mawakili wawili wa kujitegemea, umeieleza Mahakama ya Hakimu Kisutu kuwa upelelezi umekamilika.

Washtakiwa hao Bernad Bougault ambaye ni raia wa Ufaransa, Respicious Mukandala na Simphorian Kitare, walifikishwa mahakamani hapo wakituhumiwa kwa kosa moja.

Wakili wa serikali, Tuli Helela, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Francis Mhina, wakati kesi hiyo ilipopelekwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia upelelezi umefikia hatua gani.

Helela alidai kuwa kesi ililetwa kwa kutajwa na upelelezi umekamilika, hivyo wanaiomba mahakama iwapangie tarehe ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mhina aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 29, mwaka huu, kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo hayo. Februari 18, 2020 katika mtaa wa Samora, washtakiwa hao wanadaiwa walighushi nyaraka hizo.

Ilidaiwa kuwa nyaraka hizo zilionyesha kuwa Kapteni Phillipe Gerniers amemchagua Boulgault kuwa mwakilishi wake kisheria na wakala wake huku akijua si kweli.

Katika hati hiyo ilionyesha Gerniers amempa Boulgault mamlaka ya kufungua mashtaka kwa ajili ya mali zake zilizoko katika Hoteli ya Bagamoyo Beach au alipwe cha Dola za Marekani 80,000 kwa niaba yake huku akijua nyaraka hizo si za kweli.

Washtakiwa hao wako nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho na kuwasilisha mahakamani hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Dola za Marekani 40,000.



Ofisa Msimamizi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Morgan Isdor (kulia), akichukua taarifa za mlipakodi wa eneo la Ruaha, wilayani Kilosa, wakati wa Kampeni ya Elimu kwa Mlipakodi ya mlango kwa mlango mkoani Morogoro, jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# CCM yaonya makada kupanga safu 2025

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Masasi, kimewaonya baadhi ya makada wa ngazi ya juu wa chama hicho kuacha kutengeneza makundi ndani ya chama kwa makusudi ya kutaka wateuliwe kwenye nafasi walizo nazo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Onyo hilo lilitolewa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, Edward Mmavele, alipokuwa akifungua kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Masasi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Mmavela alisema katika kuelekea uchaguzi mkuu ndani ya chama mwaka huu, wako baadhi ya makada na baadhi ya viongozi ndani ya chama wameanza kupanga safu zao ngazi ya matawi na kata ili kujitengenezea fursa ya kutaka mwaka 2025 waendelee kuteuliwa kupitia makundi hayo. Alisema CCM kwa sasa inaelekea katika uchaguzi ngazi mbalimbali kuanzia mashina, matawi, kata, wilaya, mikoa hadi taifa, hivyo wanachama wanahimizwa kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho.

Katika uchaguzi huo, CCM ndani ya Wilaya ya Masasi hali imekuwa tofauti kidogo baada ya baadhi ya makada wa chama hicho hasa wale wa ngazi ya juu ambao wana nafasi, wameanza kupanga safu za uongozi ili kujiwekea mazingira rafiki ya kutaka hata na wao katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kuchaguliwa kwa urahisi.

Mmavele alisema kutokana na hali hiyo, CCM Wilaya ya Masasi inatoa tahadhari kwa makada hao kuacha mara moja tabia hiyo kwa kuwa kufanya hivyo wanatengeneza makundi ndani ya chama.

Alisema uchaguzi huo wa ndani ya chama unapaswa kufanyika kwa kufuata taratibu zote za uchaguzi na kwamba watakaonekana wanatengeneza makundi kupitia uchaguzi huu, watachukulia hatua kama chama kinavyofanya kwa kujibu wa kanuni zake.

Alisema kama wapo baadhi ya makada hao ambao wanatumia uchaguzi wa ndani ya chama kupanga safu zao za uongozi kwa maslahi yao, wajue na wao hawatarudi tena kwenye nafasi zao kwa kuwa majina yao yatakatwa.

Mmavele alisema Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya inatoa onyo kali kwa baadhi ya makada wanaofanya kazi kuacha kupanga safu badala yake wafanye uchaguzi kwa uadilifu na uaminifu.

Katibu wa CCM Wilaya ya Masasi, Didas Zimbile, alisema chama kitafuata taratibu zote za uchaguzi na kwamba uchaguzi huo utafanyika kwa amani na utulivu.

# Serikali yasaka njia bora mikopo wachimbaji wadogo

SERIKALI imesema inaangalia namna bora ya kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo wa madini nchini, ikiwamo kutumia leseni zao.

Hatua hiyo inatokana na tathmini ya utaratibu wa utoaji mikopo kwa kundi hilo iliyofanyika awali na kuonyesha upotevu wa fedha hizo.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko alibainisha hayo jana bungeni jijini hapa alipojibu swali la Mbunge wa Mbongwe (CCM), Nicodemas Maganga.

Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itawawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mikopo katika Wilaya ya Mbogwe.

Katika majibu yake, Dk. Biteko alisema kuwa awali serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwaongezea mitaji ili wafanye shughuli zao kwa tija.

"Tathmini ya utaratibu huo ilionyesha upotevu wa fedha hizo. Kufuatia tathmini hiyo, serikali inaangalia namna bora ya kuwapatia mikopo," alisema.

Dk. Biteko alisema serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) imeingia makubaliano na benki za CRDB, NMB na KCB kwa ajili ya kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, alihoji mkakati wa serikali wa kuwaendeleza wanawake wanaochimba madini kwa kuwapatia mikopo.

Waziri Biteko akijibu swali hilo, alisema kundi kubwa la wanawake limejiingiza kwenye uchimbaji madini na kwenye maeneo wanakochimba, ni waaminifu, wanaolipa kodi kwa wakati na hawahitaji kusimamiwa na polisi.

Alisema serikali inaangalia utaratibu bora zaidi wa utoaji mikopo kwa wachimbaji ikiwamo wanawake.

"Tunafanya utafiti kwa sababu kinachowekwa kama dhamana ya kupata mikopo tungetamani iwe leseni ambayo anapewa, hivyo tunahitaji kuliangalia ili yasitokee kama tuliyokosea huko nyuma ya kuwapatia watu mikopo na baadaye wakapotea na mikopo yenyewe," alisema.



Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, akizungumza wakati akiongoza kikao cha 30 cha mkutano wa saba wa Bunge la Bajeti, unaoendelea jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Msongamano wa magari mijini watafutiwa ufumbuzi

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imeliarifu Bunge kuwa serikali ina mpango kabambe wa kupunguza misongamano ya magari kwenye miji, ukiwamo Mkoa wa Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapo alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee.

Mdee alisema kwa kipindi kirefu kumekuwapo mchakato wa upanuzi wa barabara ya New Bagamoyo na Old Bagamoyo kwa lengo la kuondoa foleni kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

"Kutoka Tegeta Kibaoni hadi Daraja la Bagamoyo kwa upande wa New Bagamoyo na kwa Old Bagamoyo kutoka Morocco hadi Afrikana. Ninataka nijue lini mchakato huu utaanza kwa sababu umekuwapo kwenye mipango muda mrefu na utekelezaji umekuwa finyu, lini zitapanuliwa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Kasekenya alisema katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha, barabara hizo zimeainishwa kuwa za kipaumbele ili kujengwa kwa barabara nne au sita ili kupunguza msongamano.

Alisema taratibu zinaendelea na fedha zitakapopatikana ujenzi utaanza.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum, Anatropia Theonest, alihoji ni lini barabara inayotoka Karagwe kupita Nkwenda hadi Murongo itatengenezwa kwa lami ili kuwasaidia wakulima wanaosafirisha mazao yao kwa kutumia barabara.

Naibu Waziri Kasekenya, akijibu swali hilo, alisema zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande cha Kyerwa-Chonyonyo chenye urefu wa Km 50 imetangazwa na kufunguliwa Mei 10, 2022.

Alisema kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Moustache hadi Chonyonyo yenye urefu wa Km 12 na Kyerwa hadi Murongo yenye urefu wa Km 63, serikali ipo kwenye hatua ya ununuzi ya kumpata mhandisi mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hizo.

# Mbunge ataka mabadiliko udahili wa kidato cha tano

MBUNGE wa Meatu (CCM), Leah Komanya, ameitaka serikali kubadilisha utaratibu wa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano ili asilimia 50 ya wanafunzi watoke ndani ya halmashauri katika shule za kata.

Wakati wa maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema mpango wa utoaji elimu msingi bila malipo, umeibua vijana wenye vipaji wanaotoka kwenye mazingira magumu.

"Kwa mfano, Bariadi kuna kijana alipata 'A' zote kwenye mitihani lakini serikali imekuwa ikiwapangia shule zilizo mbali zaidi na kushindwa kumudu gharama, serikali ina mpango gani wa kuwabaini wanafunzi wa aina hii ili kuwasaidia watoto hao?" Alihoji.

Pia alihoji mpango wa serikali kujenga shule za bweni kwenye wilaya au mkoa ili kuwaokoa wanafunzi wanaokatisha masomo kutokana na kutembea umbali mrefu kwenda shule walizopangwa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, akimjibu mbunge huyo, alisema lengo la serikali kuchanganya wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ni kujenga utaifa.

Alisema kuchanganya wanafunzi kunasaidia mwanzo wa nafasi zilizopo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliofaulu wanapata nafasi ya kujiunga kidato cha tano.

"Kutumia wanafunzi asilimia 50 kujiunga na shule za sekondari ndani ya halmashauri yao kutasababisha baadhi yao kukosa nafasi kwa kuwa siyo kila mchepuo unapatikana kwenye shule zilizopo katika halmashauri," alisema.

Alisema wanafunzi wote wenye vipaji serikali inawazingatia na kwamba kama ikitokea mwanafunzi amechaguliwa eneo ambalo hastahili, ofisi hiyo imetoa nafasi ya kubadili.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, serikali ilipeleka fedha za ujenzi wa shule 10 za kimkoa za bweni za wasichana na mwaka ujao 2022/23 zimetengwa fedha kwa ajili ya shule zingine 10 ambazo zitapokea wasichana wenye vipaji katika mikoa husika.

Mbunge wa Kalenga (CCM), Jackson Kiswaga, alihoji ni lini serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Kalenga iliyoko Kata ya Ulanda kuwa ya kidato cha tano na sita.

Silinde, akijibu swali hilo, alisema maelekezo ya serikali ni kuwa na shule ya kidato cha tano na sita katika kila tarafa zikiwamo tarafa zilizoko katika Jimbo la Kalenga.

"Serikali inatafuta fedha katika mwaka 2022/23 za ujenzi wa bweni la wanafunzi ili kukamilisha vigezo vya kupandishwa hadhi shule hiyo kuwa na kidato cha tano na sita," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji


Ukurasa 12

CCBRT yaadhimisha Siku ya Fistula, kila mwaka inaponya wahitaji 462


Ukurasa 13

NDOTO YA IGP INATIMU....
Afande Mutafungwa aorodhesha staili za kufuta vifo, majeruhi barabarani


Ukurasa 14

**Miaka tisa msanii maarufu injili asaka mtoto, akihisi 'ndoa baibai'**

# Vijue 'vibanda umiza'; sumu mpya inayodhuru watoto kwa kasi kubwa

**Na Pankras Luoga**


HIVI sasa kila mahali kumesheheni maeneo ya starehe na burudani, ambavyo wenyeji wamevibatiza jina 'vibanda umiza', vingi mitaani mijini, pia vijijini.

Ni aina ya vibanda vyenye umaarufu wa kuwa vituo vya kuonyesha burudani za video, pia zaidi ni michuano ya soka, kitaifa na kimataifa, hali kadhalika sinema.

Mara nyingi maeneo hayo huwa siyo rasmi.

Kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo ongezeko kubwa la vibanda vya namna hiyo karibu maeneo yote ya nchi, hasa yanayoendelea kukua kiuchumi na kimiundombinu, kwani ni aina ya biashara ndogo inayoshamiri katika miji kama vile Iringa, Mbeya, Arusha, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba, aina hiyo ya vibanda kwa sasa vimeenea hadi maeneo ya vijijini ambako zamani huduma nyingi hazikufikika kirahisi. Inaweza kuwa zao la mapenzi ya watu wengi kwenye picha za video hasa tamthilia mbalimbali, pia michezo mbalimbali na hasa mpira wa miguu.



Ndivo yalivyo maisha ndani ya 'vibanda umiza'. **PICHA; MTANDAO**

### VINAVYOFANYA KAZI

Vibanda hivyo vya video hupokea wadau wote pasipo kujali umri, ikigusa hata wanafunzi wa ngazi mbalimbali za masomo, pia kipato au haiba ya anayeenda kuangalia. Cha msingi kwao, ni uwezo wa kulipa kiingilio au kununua chochote, hasa vinywaji kama soda katika kipindi cha kushuhudia.

Watoto hao wanajulikana hawana chanzo chochote cha kipato kwa sasa, hivyo hawamudu gharama za kuangalia video au mpira, yaani kulipa kiingilio au kununua vinywaji.

Hapo ndipo wazazi na jamii wanapoanza kunyooshewa kidole cha kutengeneza mazingira ya watoto wao kuchukua fedha nyumbani bila ya taarifa au kuficha kiasi cha fedha wanapotumwa kununua mahitaji ya nyumbani, au kwa ajili ya shuleni.

Pia, kuna hali nyingine watoto wanafikia hatua kukubali kulipiwa gharama za huko 'vibanda umiza' kwa maana ya msaada na watu wanaowajua au wasiowajua na maeneo hayo nayo yanatajwa siyo rafiki kwa afya ya akili, kwani yamekuwa yakitawaliwa na vurugu, pia vitendo visivyokubalika kijamii na kauli zisizofaa kwa umma.

Baadhi ya watu huanza kutukanana na kupigana pindi timu zao zikipata matokeo yasiyoridhisha kama vile kufungwa. Hiyo inaendana na hali wakishakunywa na kulewa, wanaleta vurugu kuwafanyia vitendo mbalimbali bila wao kujielewa, ikiwa ni pamoja na watu wa ama jinsia moja au tofauti, kuanza kushikana au kuongea kimapenzi.

### SURA YA ATHARI

Watoto wanaanza kujifunza wanayoyaona kuanzia ya video na kwa wanajamii, wanayafanya kipindi cha kuangalia video au mpira, kama vile matusi, chuki, kupigana na mapenzi.

Ndiyo maana uzoefu wa kupita mitaani, watoto wengi wanaiga wanayoyaona kwenye video kama vile kupigana na kutumia bunduki na bastola za miti. Tukumbuke msemo wa kiingereza 'no free lunch" kwa maana "hakuna kitu cha bure". Watoto wanaosaidiwa kulipiwa kuangalia video au mpira lazima walipe.

Je wanalipiwa nini? Kimsingi, ni hali kwa baadhi ya watoto kulipiwa na watu kwa njia ya msaada, maarufu kwa jina la 'wajomba' na 'kaka wa hiari" hutoa mwanya kwa watoto kuingia kwenye mitego miovu kama vitendo vya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto kama ubakaji na ulawiti, kutukanwa na kudharauliwa.

Mwisho hufanya watoto kupata mimba za utotoni, kushindwa kufanya vizuri katika masomo na kuacha shule na kujiunga na makundi yasiyofaa katika jamii kama vile 'Panya Road'.

Pia, kwa baadhi ya watoto huanza tabia ya kuiba hela nyumbani ili kuweza kumudu gharama za kuangalia video au mpira.

Pale tabia hizo kama zisipofuatiliwa au kugundulika mapema hata zikakomeshwa, zinajengeka zaidi kadri muda unavyosonga, hata kuwapo tabia kamili na mazoea.

### KINGA IKOJE?

Wazazi na walezi katika jamii kwa ujumla, wanawajibika kuhakikisha wanaimarisha tathimini na ufuatiliaji wa karibu wa watoto, ili kuhakikisha watoto wao hawaendi katika maeneo hayo ya video na mpira, badala yake wanatumia muda wao kusoma na kujifunza yanayoweza kuwa na faida zaidi maishani mwao.

***• Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili (MUHAS) na anapatikana kwa simu:+ 255 757 645746.***

AFYA

# CCBRT yaadhimisha Siku ya Fistula, kila mwaka inaponya wahitaji 462

## • Yaomba upendeleo kupokea wagonjwa wake



Maandamano yakifanywa na waliopona maradhi ya fistula, baada ya kutibiwa hospitalini CCBRT. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Yasmine Protace**

UGONJWA wa fistula una tafsiri kitaalamu kuwa tundu lisilo la kawaida kati ya kibofu cha mkojo na faragha ya mwanamama, njia ya haja kubwa na ndogo.

Matokeo ya tatizo la fistula ni kwamba, mwanamke anapata shida ya kutokwa na haja ndogo au kubwa, au vyote kwa pamoja katika namna isiyo ya kawaida na hana uwezo wa kujizuia.

Sababu kuu ya fistula ni pale mwanamama anapata tabu katika hatua ya kujifungua, pasipo kuwapo huduma ya haraka.

**TIBA NA KUZUIA**

Kitaalamu inaelezwa, hutokea katika hatua za mama kujifungua na matibabu yake huwa, mgonjwa kufanyiwa upasuaji na uponyaji wake unachukua wastani wa wiki mbili.

Inaelezwa, jinsi ya kuzuia fistula ya uzazi, inaanzia kwa mjamzito kuhudhuria kliniki ili kufuatilia maendeleo ya ujauzito hata akapatiwa ushauri sahihi.

**KUTOKA CCBRT**

Mkurugenzi Mtendaji wa CCBRT, Brenda Msangi, katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Fistula yaliyofanyika katika Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam anasema kila siku ya Mei 23 ya mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku ya kimataifa ya kutokomeza fistula ya uzazi.

"Huu ni mwaka wa 10 tangu tulipoanza kuungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii mwaka 2013," anasema, akiongeza kaulimbiu ya maadhimisho hayo mwaka huu anaitamka kuwa

'Tokomeza fistula, Wekeza, Imarisha Huduma za Afya na Wezesha

> **Pamoja na juhudi zote hizi, nchi yetu bado inakabiliwa na tatizo la ugonjwa wa fistula. Hii inamaanisha kwamba, bado tunayo kazi ya kufanya kuhakikisha tunatokomeza ugonjwa huu.**




Mkurugenzi Mtendaji wa CCBRT, Brenda Msangi.

Jamii.'

Anaongeza kuwa ni kaulimbiu inayohamasisha CCBRT katika nafasi yao washirikiane na wadau mbalimbali, ikiwemo serikali nchini, huku wakifanya uwekezaji mkubwa.

Katika hilo, mkurugenzi huyo anafafanua kinachoendelea sasa ni kujengwa kitengo kipya cha afya ya mama na mtoto, kinacholenga kuwahudumia kinamama wenye historia ya fistula, ulemavu, pamoja na mabinti wanaopata mimba za utotoni.

Brenda anafafanua kwamba, lengo lililopo sasa ni kuzuia matukio mapya ya fistula, huku wakihudumia wenye ulemavu na kuondosha vifo vya mama na mtoto. Anasema, kwa muda mrefu CCBRT imekuwa ikiiwezesha jamii kwa kutoa mafunzo ya fistula kwa wahudumu wa afya katika jamii, wakiwemo mabalozi wa fistula kitaifa.

"Nipende kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wetu ndani na nje ya nchi wanaoendelea kutushika mkono ili kuweza kutoa matibabu, chakula, nauli na malazi bila malipo," anasema.

Pia, anaongeza kuwa tangu kuanza juhudi za mapambano dhidi ya fistula mwaka 2003, wamepiga hatua kubwa kitaifa katika kutoa matibabu ya fistula kwa maelfu ya kina mama wenye tatizo hilo jumla yao zaidi ya 17,500 walipatiwa matibabu CCBRT na katika hospitali washirika.

"Pamoja na juhudi zote hizi, nchi yetu bado inakabiliwa na tatizo la ugonjwa wa fistula. Hii inamaanisha kwamba, bado tunayo kazi ya kufanya kuhakikisha tunatokomeza ugonjwa huu," anasema.

Mkurugenzi huyo anaongeza kwamba mwaka jana wametoa matibabu kwa kinamama 462, akisema bado ni idadi ndogo sana, ikilinganishwa na ukubwa wa tatizo lilivyo.

Rai yake ni kwamba, Watanzania wanapaswa kutoa mchango katika kutokomeza fistula, kukiwapo ushirikiano wa namna na mahali huduma husika inapatikana kutibu ugonjwa huo.

Hivyo, anashauri hali iendane na kuwepo sera kitaifa zinazolenga kuboreshwa mazingira ya upatikanaji huduma bora za afya za mama na mtoto, pia sekta binafsi, ili ziwezeshe kupatikana huduma hizo nchini na kupunguza utegemezi nje ya mipaka.

**SAFARI YA WAGONJWA**

Brenda anasimulia wagonjwa wa CCBRT ambayo huwahudumia bure, wengi huwa wanafika jijini Dar es Salaam, kwa njia ya barabara na stendi yao zaidi, ni Kituo cha Mabasi cha Magufuli, kilichoko Mbezi wilaya ya Ubungo.

Anasema, wagonjwa hao wengi hufika Dar es Salaam kwa mara ya kwanza kwa kupandishwa mabasi na mabalozi wao huko mikoani, huku wao wakiwasiliana nao njia nzima kupitia makondakta wa basi husika hadi hapo wanapofika Mbezi, akiwapongeza wadau wote hususan makondakta na madereva wanaotoa ushirikiano kukubali abiria hao.

Pia, anaeleza kumekuwepo changamoto, pale mgonjwa anaposhushwa usiku kutokana na basi kuchelewa kufika, mara nyigi huwa wanahangaika kwa kuwa hawana nyenzo za mawasiliano na kuna wakati kondakta anakuwa ameshaachana nao.

Hapo anaomba wapatiwe nafasi ya kuweka dawati na nembo ya CCBRT mahali hapo, ili wawe wanaelekezwa sehemu ya kumsubiri dereva wa hospitali anayewafuata kituoni hapo.

**MWENYE SIMULIZI**

Ana Michael mkazi wa jijini Dodoma, anasema yeye alipata fistula baada ya kujifungua na sababu kuu inatokana na kuongezwa njia ya kujifungua kienyeji, kwa kuchanwa na wembe.

Anasema baada ya siku ya tatu kufika ndipo alipata maumivu makubwa kutokwa na mkojo na haja kubwa kila mara kwa kipindi kirefu. Mkurugenzi wa CCBRT, anafafanua kwamba baada ya kupelekwa hospitali, ndipo alipogundulika kuwa na fistula na akafikishwa CCBRT kwa ajili ya matibabu na sasa amepona.

**RMO WA DAR**

Mganga Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, anasema elimu inatakiwa kuendelea kutolewa, ili jamii ijue madhara ya ugonjwa fistula.

Dk. Mfaume aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, anaungana na hoja fistula ya uzazi ni tatizo kubwa na zaidi ya watu milioni mbili duniani wanaishi na ugonjwa huo, akiipongeza CCBRT kwa kutoa matibabu bure, pia kugharaimia nauli zao.

AFYA

NDOTO YA IGP INATIMU....

# Afande Mutafungwa aorodhesha staili za kufuta vifo na majeruhi barabarani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BADO kuna kumbukumbu wakati fulani, aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Saidi Mwema, alitamka katika ripoti yake muda mfupi baada ya kutumikia wadhifa wake, kwamba amefanikiwa katika kukabili uhalifu ikiwamo ujambazi, ila bado aliumizwa kichwa na ajali za barabarani.

Huko alinuia kukamia kwa vita vikali, ambako kuliendana na madhara, pia vifo kwa umma wa wasafiri na watembea kwa miguu, nyenzo kubwa za madhila hayo ni vyombo vya moto; magari, pikipiki, bajaji, baiskeli na guta.

Leo hii, aliyekalia kiti chake sasa, IGP Simon Sirro anaendeleza ndoto ileile ya mstaafu Mwema, akitangaza kufanyika operesheni wa ukaguzi wa vyombo vya moto mwezi mzima, kudhibiti ajali za barabarani, ikiendana na angalizo, dereva atakayebainika kuvunja sheria anachukuliwa hatua kwa kufikishwa mahakamani.

Hata hivyo, hilo siyo geni, kwani ukaguzi wa vyombo hivyo umekuwa ukifanyika kila mara katika vituo vikubwa vya mabasi yaendayo mikoani, barabarani na magari yanayopatikana kuwa na dosari katika mifumo ya breki, matairi vipara na kuharibu ving'amuzi, yanazuiliwa kuendelea na safari.

Zao lake, tangu kukerwa kwa Afande Mwema, leo akiwa mstaafu inatia majibu, kwamba ajali zinapungua na ikitoa taswira kwa wananchi na wanaoendesha vyombo hivyo, kwamba wanazingatia alama na sheria za barabarani, licha ya kwamba baadhi yao, wenzao wamekuwa wakikaidi.

Ripoti ya utafiti mmojawapo uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kukabidhiwa kwa serikali, imebainisha kuwa robo tatu ya ajali za barabarani zinachangiwa na tabia za madereva.

Hiyo inafanyika, huku IGP Sirro ameshawaagiza makamanda wa polisi wa mikoa, wafanye operesheni ya ukaguzi wa vyombo vya moto mwezi mzima, kudhibiti ajali za barabarani na madereva.

"Madereva wanapofanya kosa na kulipa faini mahakamani mara kwa mara, mwisho wa siku makosa ya barabara yataonekana hayana nguvu, lakini niwahakikishie haya makosa ya barabara yanaua kuliko makosa mengine, lazima tutakuwa wakali sana kwa hili," anatamka IGP Sirro.

Hata hivyo, ripoti ya jeshi la polisi inaonyesha matukio ya ajali barabarani yamepungua, ikilinganishwa na vipindi vingine kutokana na kuwepo elimu inayozidi kutolewa na wanaoenda kinyume kuchukuliwa hatua kukomesha tabia zao.

Ripoti hiyo ya Polisi inaonyesha, mwaka 2019 kulikuwapo ajali za jumla ya malori 874 hata kusababisha vifo vya watu 272 na majeruhi 271; mwaka juzi 2020 ajali zilikuwa 458, vifo vilikuwa 147 na majeruhi 152. Aidha, kwa mwaka ulipita, kulikuwapo jumla ya ajali 169 kitaifa na kuchangia kupotezwa maisha ya watu 47 na majeruhi 66



Malori yakiwa safarini. **PICHA: MAKTABA**



Mkuu wa Polisi, Usalama Barabarani, SACP Wilbrod Mutafungwa, alipozungumza na wanahabari, baada ya kukagua magari ya abiria na mizigo katika barabara kuu. **PICHA: SHABAN NJIA**

### AFANDE WA TRAFIKI

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi (SACP), Wilbrod Mutafungwa, anasema madereva wa magari ya mizigo wanaosafirisha abiria watachukuliwa hatua, kwa sababu wamekuwa chanzo cha vifo kwa watu wasiokuwa na hatia.

Anasema operesheni ya kudhibiti makosa na kuzuia ajali za barabarani inaendelea nchi nzima, ikitarajiwa itasaidia kupunguza ajali za barabarani na matokeo yanaonekana, baada ya madereva kuanza kuzingatia sheria na alama za barabarani wawapo safarini.

SACP Mutafungwa anasema, katika operesheni hiyo, wanatumia vifaa vya kudhibiti mwendo kasi, mifumo anayoitaja ya 'veiko, vipimo vya ulevi na mipango kazi thabiti ya kiaskari kukagua kila mara na dereva anayeonekana sugu wa makosa hayo, atafungiwa leseni ya kuendesha chombo cha moto.

Kamanda huyo anasema, kwa sasa matunda yameanza kuonekana kutokana na elimu ya usalama barabarani inayotolewa nchi nzima na askari wake, madereva wengi wanabadilika, hivyo kuleta matumaini makubwa ya kupungua ajali.

Anafafanua kwamba, ukaguzi uliofanyika wilayani Gairo mkoani Morogoro hadi Kanda ya Ziwa, iliyafikia jumla ya mabasi 173 na kati yao 87 yalifuata utaratibu wa usalama barabarani; 47 yalitozwa faini; tisa waliyaonya; manane yalikuwa yamezima ving'amuzi; na mengine hayakuwa na breki na matairi vipara.

Kwa mujibu wa SACP Mutafungwa, kuna magari 15 yalikuwa ni mabovu yakiwa na abiria, waliyazuia kuendelea na safari mpaka pale yatakapotengenezwa na kukaguliwa na askari.

Vilevile anasema, magari mengi yamekuwa yakipata ajali kutokana na sababu kama za ulevi barabarani, mwendokasi, kuzidisha abiria na utaratibu wa abiria kupanda magari ya mizigo, hali iliyo kinyume na sheria.

> Wenye tabia ya kubeba abiria katika gari hilo, ni kwamba madereva wa kitanzania, lakini madereva wa kigeni hawana tabia hizo kwa sababu sheria zinawabana sana.

### ALAMA ZA BARABARA

SACP Mtafungwa anasema kupitia wadau wa barabara wa serikali kama vile Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), wamewasaidia kuweka alama sahihi na salama zinazoonyesha matumizi ya barabara na wanaokiuka huchukuliwa hatua.

"Tuna utaratibu wa kuweka polisi wa kutosha barabarani, utaratibu huo tunauita 'high police visibility'. Kuna askari wanapangwa kufanya doria za magari kila baada ya kilomita fulani na wengine wanakuwa kwenye 'check points' (vituo maalum vya ukaguzi), hivyo ni wajibu kuheshimu alama za barabarani.

"Kuna kipindi tunalazimika kupima ulevi kwa kila dereva aliyepo barabarani hasa nyakati za sikukuu na alfajiri na nyakati hizo tunakuwa makini kuliko kawaida, kwa sababu watu wanajisahau na kuvunja sheria kwa makusudi na kuwa na ajali nyingi," anaeleza SACP Mutafungwa.

### MADEREVA MALORI

Dereva wa magari makubwa yaendayo nchi jirani za Rwanda, Omary Juma, anakiri kuwepo baadhi ya magari ya mizigo kubeba abiria na sababu kubwa ni baada ya kuishiwa fedha za matumizi walizopewa na mabosi zao, hivyo wanatafuta fedha za matumizi njiani.

Dereva mwingine, William Mashamba, anasema wenye tabia ya kubeba abiria katika gari hilo, ni kwamba madereva wa kitanzania, lakini madereva wa kigeni hawana tabia hizo kwa sababu sheria zinawabana sana.

Anaeleza, kwa sasa wanatumia barabara vizuri hata vikikosekana vibao ambavyo vimekatwa na watu wasiokuwa waadilifu katika baadhi ya maeneo ambapo vibao hivyo vinawafanya kupunguza mwendo.

AFYA

# Miaka tisa msanii maarufu injili asaka mtoto, akihisi 'ndoa baibai'

• Kejeli: Unaimba 'waweza'halafu huwezi

Na Mwandishi Wetu

***"...Nilikuwa ziarani Marekani ... nilianza kutamani vyakula vya ajabu sana, hadi nilikuwa nakula barafu. Ni kitu kilichonishangaza sana, hadi nilipofanya vipimo nikathibitishwa..."***

EVERLYNE Wanjiru ni mwanamama maarufu sana katika nyimbo za injili, akiwa na mashabiki lukuki, hata kumliwaza sana.

Hata hivyo, upande wa pili wa shilingi imemchukua muda mrefu kuwa na uchungu wa siri, kutokana na mahangaiko ya kupata ujauzito kwa miaka tisa ya ndoa yake.

Mara ilipofikia hesabu ya mwaka wa tisa ya ndoa yake, mtumishi huyo wa kiimani kupitia sauti na sanaa yake, akahamishiwa upande wa faraja, pale aliposhuhudia kuwa na ujauzito mwaka huo na kufanikiwa kujifungua mtoto wa kiume.

Ushuhuda wake umebeba kauli hii:"Kwanza kabisa nataka kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunitoa aibu na kutupangusa machozi ya miaka mingi mimi na mume wangu.

"Tulihangaika kwa siri tukitafuta njia ambayo ingenihakikishia kushika mimba na mwaka wa 10 wa ndoa yetu, siamini kwamba ninampakata mtoto wangu mikononi - huu ni muujiza."

**KUTAWALIWA NA SHAKA**

Anaendelea 'kufunguka' lingine la moyoni, kwamba akiwa na shaka kwamba yeye ni msanii wa nyimbo za injili, zenye lengo la kutoa matumaini kwa watu katika maisha yao, lakini majibu hayo hayaonekani katika maisha yake binafsi .

Everlyne anatoa mfano wimbo mojawapo ambao ni maarufu unaoitwa 'Waweza' ulionekana mithili ya kejeli kuu katika maisha yake, wakati anaimba Mwenyezi Mungu anaweza yote, ilhali kwake inakwama.

"Kwenye maisha haya tunayoishi hasa mila za Kiafrika, jamii inatizama kila wakati panapokosekana mtoto, huwa mwanamke ndio ana shida. Kwa hiyo, mara tu unapoolewa hata bado mko kwenye fungate, wameanza uliza vipi mtoto?" anasimulia Everlyne.

"Kwa hiyo imekuwa safari ngumu, pia safari ya kutia moyo kila siku, kwa ndoa yangu nilikuwa najipa moyo kwamba siku moja Mungu atanitendea,"anasema Everlyne, akidokeza kilichoendelea nyuma ya pazia, baadhi ya watu walikuwa wanamsimanga .

Akiwa msanii wa nyimbo za injili na akitumia mitandao ya kijamii katika kueneza nyimbo zake, anasema amekutana na maoni ya baadhi ya watu ambayo yangemshusha, kwa mfano maneno anayonukuu, huku akilalamika hatoyasahau: "Wewe bure sana, nenda ukazae kwanza! "



Everlyne Wanjiru, akiwa na mumewe na mtoto wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**"Baadaye yeye na mume wake walipoenda hospitalini, daktari alimfahamisha kwamba alikuwa na matatizo katikia afya ya kike mwilini mwake.**



Everlyne alipokuwa mjamzito.

**HOFU KUPOTEZA MUME**

Pia, Everlyne anasema, ndani ya ndoa nako kila kukicha alikuwa na wasiwasi sana kuhusu hatma ya ndoa yake, akihofu uamuzi wa mume wake.

Anarejea alivyojiuliza: "Je, huyu mume wangu kipenzi changu atasubiri hadi lini?" Ni aina ya mawazo yaliyomjia kwa kuona miaka ya ndoa yao inasonga kwa kasi na huku hawajajaliwa mtoto.

Pia, anakumbusha hofu moyoni kuhusu mustakabali wa mazingira ya utamaduni wa Kiafrika, ambazo nyingi zinaamini kuwa mwanaume aliyeoa ni sharti apate watoto, tena wengi.

"Ninafurahia na ninafahamu kwamba, mume wangu alinipenda na alikuwa amesimama na mimi katika harakati za kutafuta kila njia ya kupata ujauzito. Ila, nilikuwa na wasiwasi kwamba ninaweza kumpoteza!

"Unajua mila zetu zilivyo hasa kwa upande wa wanaume walioko kwenye ndoa, kwamba wake wao wawe na uwezo wa kuwapa watoto .Sasa mimi nilikuwa nauliza, Mungu itakuwaje sasa miaka ndio hii inasonga bila mafanikio yoyote, "anakumbuka Everlyne

Katika harakati za kupata mtoto, mama huyo na mumewe wakaamua waanze kutafuta tiba au hata ushauri kutoka kwa wahudumu wa afya ya uzazi, kuhusiana na kutopatikana ujauzito.

Anarejea alipotupa ratiba alikotoka, anakumbuka kuna wakati kalenda zake za kike hazikukaa sawa, lakini akapuuzia kama ni la kawaida, pasipo kujua kulikuwapo walakini kiafya. Hata hivyo, akapata mwamko na kuchukua hatua stahiki kusaka ushauri wa kiafya.

Baadaye yeye na mume wake walipoenda hospitalini, daktari alimfahamisha kwamba alikuwa na matatizo katikia afya ya kike mwilini mwake.

Ni wakati huo ndio akaanza safari yake kusaka matibabu mbalimbali na akapatiwa dawa za kumsaidia katika mifumo yake ya uzazi na maumbile kwa miaka miwili, hata siku moja akajigundua ana ujauzito (mwaka jana).

"Nilikuwa ziarani Marekani, niligundua kwamba kuna baadhi ya harufu zilikuwa zinanipa shida wakati huohuo, pia nilianza kutamani vyakula vya ajabu sana, hadi nilikuwa nakula barafu. Ni kitu kilichonishangaza sana, hadi nilipofanya vipimo nikathibitishwa mimi ni mjamzito," anakumbuka Evelyne

Ni kuanzia hatua hiyo, anasema siku zote zilizofuata baada ya hapo zikawa za furaha sana, akielekeza shukrani kwa Mwenyezi Mungu hadi Aprili tarehe 6 mwaka huu, alipojifungua mtoto wa kiume ambaye wamempa jina Mshindi, hali anayoitaja inampatia fahari kuu, hususan ndani ya jamii yake .

Wito wake mkuu sasa kwa umma, umekuwa ujumbe "subira huvuta heri maishani" na kwamba "wakati walimwengu wanang'ang'ana kutafuta mali , watoto au chochote wasiwe na haraka au kukata tamaa."

***• Kwa mujibu wa BBC.***

## Minara 670 kujengwa ndani ya mwaka mmoja

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilion 70 kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa huku ikitarajia kujenga minara 673 ndani ya mwaka mmoja ili kuboresha miundombinu ya mawasiliano nchini.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Methew Kundo, alibainisha hayo juzi wakati wa mdahalo wa Wiki ya Ubunifu uliofanyika jijini hapa.

Katika mdahalo huo ulioandaliwa na kampuni ya mawasiliano ya simu ya Vodacom Tanzania, Naibu Waziri Kundo aliwataka wananchi kutumia fursa zinazowezeshwa na serikali ili kufanya maendeleo binafsi ikiwamo kujiinua kiuchumi.

Alisema mipango ya serikali ya kuboresha miundombinu ya mawasiliano nchini itawezesha ubunifu wa mtandao na kwa gharama nafuu.

Naibu Waziri alisema ubunifu huo wa mtandao wa vitu unalenga katika kuiwezesha jamii kupata kila kitu inachohitaji mahali ilipo bila kulazimika kusafiri kukifuata.

"Miundombinu ya mawasiliano ikikaa vizuri, ni lazima ubunifu wa mtandao utakaa vizuri, ndiyo maana serikali inawekeza kwenye uboreshaji wa miundombinu," alisema Kundo.

Alifafanua zaidi ya kuwa mawasiliano mazuri ya mtu anayetumia barabara isiyo na lami yenye mabonde, itamfanya kusafirisha vitu kwa muda mrefu na kwa gharama kubwa lakini kwa kutumia lami, atasafirisha vitu kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

"Hivi ndivyo mfumo wa mawasiliano unatakiwa kuwa, ndiyo maana kila uchao serikali inawasisitiza watoa huduma hiyo kuboresha mazingira ya mawasiliano," alisema Kundo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuhakikisha mtumiaji wa mwisho anapata mawasiliano kwa gharama nafuu na ndiyo maana anawekeza kwenye miundombinu.

Alisisitiza kuwa mtandao wa vitu unawezesha kupata taarifa na kutumia taarifa na kuzilinda kwa kutumia huduma ya mawasiliano na ndiyo sababu serikali imekuwa ikisisitiza uboreshwaji wa huduma za mawasiliano kwa watoa huduma hizo.

"Sisi ambao ni walezi wa sekta hii tutaendelea kukaa na kampuni zote na taasisi zote ambazo zitakuwa pamoja nasi kwenda kufikia malengo ya kukamilisha mradi wetu wa kuwafanya Watanzania kufikiria zaidi kidijitali," alisema Kundo.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Rosiline Moria, alisema teknolojia ya mtandao wa vitu imewezekana kwa sababu ya sera ya miundombinu iliyowekwa na serikali.

# Bil. 500/- kutatua umeme kukatika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) katika mwaka wa fedha 2022/23 limeomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 500 kwa ajili ya kutatua tatizo la uchakavu wa miundombinu linalosababisha umeme kukatika mara kwa mara.

Akizungumza jana kwenye maonyesho ya Wizara ya Nishati na taasisi zake yanayofanyika kwa siku tatu kwenye viwanja vya Bunge mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema:

"Kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati itakayojadiliwa bungeni Juni 2 na 3, mwaka huu, baadhi ya fedha tulizoomba ni za kutatua changamoto ya miundombinu ambayo inasababisha umeme kukatika.

"Kuna fedha kama Sh. bilioni 500 ambazo tunaenda kuomba idhini na hizo zitatoa majawabu ya miradi mbalimbali ile njia ndefu ya Mpwapwa, Kiteto, Chanika kule Dar es Salaam, Songwe na maeneo mengine mengi."

Alisema kwa sasa hakuna mgawo wa umeme na takwimu za Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zilionyesha ukame kwa mwaka jana.

"Asilimia 35 ya vituo vyetu vya kuzalisha umeme vinategemea maji, kwa hiyo tulipata upungufu wa uzalishaji umeme na kusababisha baadhi ya maeneo yaathirike lakini tulikuja na mpango wa kuongeza nguvu ya uzalishaji wa gesi na tuliahidi kuweka kituo namba tatu cha Ubungo Megawati 112 tulifanya hivyo, na sasa hivi tukasema tutaweka kituo cha Kinyerezi namba moja Megawati 185, tunawasha mitambo kwa majaribio mwezi ujao," alisema.

Alibainisha kuwa inatarajiwa mwezi Novemba mwaka huu mradi wa Kinyerezi utakamilika.

"Pia kwenye mradi wetu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, yote haya ni kuhakikisha suala la uzalishaji umeme linaongezeka,"alisema.

Kuhusu maonyesho hayo, mkurugenzi huyo alisema wanatoa taarifa kwa wabunge kuhusu uzalishaji na usafirishaji wa umeme.

"Kuna mabanda hapa yanazungumzia vituo vyetu vya uzalishaji kama Kidatu, Kihansi na kadhalika, pia miradi mikubwa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, ukifika hapa hakuna swali ambalo litakosa jawabu," alisema.

Katika hatua nyingine, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema umeme ukifika kila kijiji na maeneo yote yenye vivutio vya utalii, utasaidia kuvutia wawekezaji.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo jana, Dk. Tulia alisema: "Ile filamu ya The Royal Tour watalii wengi watakuwa wanakuja, sasa mtalii kuanza kumweka tena kwenye kibatari, sawa inawezekana lakini kwao kaishazoea umeme.

"Tuliambiwa tujiandae Watanzania kupokea wageni, ninaamini haya ndiyo maandalizi yake, watu watakwenda kila mahali, hoteli zitajengwa kwenye vivutio."



Wakazi wa Mailimbili, Kata ya Mnadani, jijini Dodoma, wakifanya usafi kando ya barabara kuu ya Dodoma- Arusha juzi, kwa ajili ya kuliweka jiji hilo safi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Makinda asema sensa mwaka huu bora zaidi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi Tanzania Bara, Anne Makinda, amesema serikali imedhamiria kufanya sensa bora kuliko zilizopita ili kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazozalisha takwimu bora.

Makinda aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipofungua kikao cha kwanza cha kamati ya ushauri ya ufundi ya sensa. Sensa hiyo imepangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Sala zetu sisi hapa kila wakati ni kukamilisha zoezi hili kwa mafanikio ili kukidhi matarajio ya viongozi wa nchi yetu na matarajio ya Watanzania na tunataka kufanya sensa bora zaidi kuliko zilizopita," alisema Makinda.

Spika mstaafu huyo alisema kamati hiyo itahusika moja kwa moja na masuala yote yanayohusu utaalamu unaotakiwa ili utekelezaji wa sensa ufanyike kwa weledi na ufanisi huku ikizingatia miongozo ya Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu utekelezaji wa sensa.

Alisema matarajio makubwa kutoka kwa kamati ni kushauri namna watakavyoona inafaa kulingana na utaalamu, ujuzi, uzoefu , umakini na kwa ubunifu kwa kuzingatia na kuweka mbele maslahi ya nchi.

"Tukumbuke kuwa lengo kuu la kufanya sensa ni kupata takwimu bora ambazo zitasaidia kuinua kiwango cha maisha ya Watanzania kupitia sera na mipango inayoandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya kitakwimu.

"Na hili ndilo lengo la serikali yetu tangu awamu ya kwanza hadi awamu ya sita na ndiyo maana Tanzania ni miongoni mwa nchi chache ambazo zinafanya sensa ya watu na makazi kulingana na maelekezo ya Umoja wa Mataifa ambayo yanazitaka nchi kufanya sensa angalau mara moja kila baada ya miaka 10," alisema. Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alipongeza serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha sensa ya mwaka huu kufanyika kisasa zaidi.

Alisema kwa mara ya kwanza wanakwenda kutumia vishikwambi na kuachana na karatasi ambazo zilitumika katika sensa zilizopita.

"Tunampongeza Rais Samia kwa kuwezesha zoezi hili la sensa na niwahakikishie kuwa katika suala la maandalizi tumefikia pazuri hadi kufikia mwezi Agosti mwaka huu tutakuwa tumekamilisha kwa asilimia 100," alisema.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Wilson Mahela, alisema takwimu zitakazopatikana katika sensa ya mwaka huu zitasaidia katika uandikishaji daftari la wapigakura.

Alisema ni muhimu sensa ya watu na makazi ikafanyika kwa ufasaha zaidi ili Taifa lipate takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga mipango yake ya maendeleo.

"Tutakuwa na zoezi la kuandikisha daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2025, hivyo tunategemea takwimu zitakazopatikana katika sensa ya mwaka huu zitatusaidia na sisi katika zoezi letu," alisema.





# Wakulima wa mpunga wataka soko la uhakika

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAKULIMA wa mpunga wanaotumia mbolea za asili wilayani Kyela, wameiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika ambalo litawasaidia kupata bei nzuri kulinganisha na wale wanaotumia mbolea za viwandani.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wakulima hao wakati wa kikao cha kuvijengea uwezo vikundi vya wakulima wa zao hilo kutoka kata za Makwale, Ndobo na Mababu, kilichoandaliwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Jukwaa la Wadau wa Kilimo wasio wa Kiserikali (ANSAF), maofisa ugani na viongozi wa halmashauri.

Mmoja wa wakulima hao, Furaha Mwasongela, alisema mafunzo waliyopatiwa yamewasaidia kulima kilimo cha ikolojia ambacho kinazingatia utunzaji wa mazingira na viumbe hai, hivyo kupata mavuno mengi.

Alisema kilimo cha ikolojia kwenye mpunga kina tija kubwa kwa wakulima kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi ya mbolea za asili, kunasaidia kutibu afya ya udongo ambao kwa sasa umeathiriwa na matumizi ya mbolea za viwandani.

Alisema hitaji lao kubwa kwa sasa ni kutafutiwa soko la uhakika la kuuza mpunga ambao wanazalisha kwa kutumia mbolea za asili. Alisema kutokana na ubora wa zao hilo, wanapaswa kuuza kwa bei kubwa kulinganisha na ule unaozalishwa kwa mbolea za viwandani.

Naye Salome Mahusi alisema kilimo cha ikolojia kimewasaidia kutumia gharama ndogo za uzalishaji ambazo kazi yao kubwa ni kuandaa mbolea za asili ambazo ni mboji zinazopatikana kwa urahisi kulinganisha na zile za viwandani.

William Mmari, ambaye ni Mtafiti wa Udongo kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, alisema matumizi ya mbolea ya viwandani yamechangia kwa kiasi kikubwa kuharibu afya ya udongo.

Alisema kilimo cha ikolojia kimekuja kutibu afya ya udongo na kuwawezesha wakulima wa mpunga kupata mavuno mengi na yenye ubora kulinganisha na ilivyokuwa awali.

Akizungumzia bei ya mpunga ambao unazalishwa kwa mbolea asilia, Ofisa Kilimo na Ushirika Wilaya ya Kyela, Kenneth Nzilano, aliwahakikishia wakulima kuwa watafanya kikao na wanunuzi wa mpunga wakiwamo, Raphael Group kununua kwa bei kubwa kulinganisha na wanaozalisha kwa mbole za viwandani.

Alisema licha ya kupanga kufanya mazungumzo na Raphael Group, pia watafanya mazungumzo na wadau wengine kuangalia kwa jicho la karibu mpunga unaozalishwa kwa mbolea asilia.



Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Liliani Bruno (kushoto), akipongezwa kwa siku yake ya kuzaliwa na Muuguzi wa Hospitali ya Igawilo, Jenifa Kapepena, wakiwa katika mafunzo ya utoaji wa huduma ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, ili kufanikisha hamasa ya chanjo ya UVIKO-19 kwa wauguzi, watoa huduma za kijamii, viongozi wa dini na kimila na waandishi wa habari, iliyofadhiliwa na Shirika la Afya la Amref na kuratibiwa na Asasi ya PHEDES Tanzania, jijini Mbeya jana. Kulia ni Mwandishi wa ITV, Renatus Mutabuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kupanda bei kahawa kwaibua ongezeko mahitaji ya miche

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADA ya kupanda kwa bei ya kahawa nchini kutoka Sh. 4,300 hadi 7,000, mahitaji ya miche yamekuwa makubwa kulinganisha na uzalishaji wa miche hali inayowaibua wataalamu kuongeza kasi ili kukidhi mahitaji.

Ofisa Ubora Mwandamizi wa Kahawa Kanda ya Mbeya, Gerald Mlay, alisema juzi kuwa kupanda kwa bei ya kahawa nchini ni matokeo ya jitihada zilizofanywa na wadau wote wanaohusika na mnyororo wa thamani.

Alisema mbali na kusaidia kutafuta soko la uhakika pia waliwajengea uwezo wakulima namna bora ya kuzalisha bidhaa hizo.

Mlay alisema kuongezeka kwa bei ya kahawa kumewasaidia wakulima kumudu gharama za maisha ikiwamo kusomesha watoto, kujenga na kufungua miradi mingine ya kujikwamua na umaskini.

Alisema kupanda kwa bei ya zao hilo kumechangiwa pia na mahitaji ya bidhaa hiyo duniani kutokana na kuzalishwa katika hali ya ubora ambao unamudu ushindani wa soko la dunia.

Alilipongeza Shirika la Cafe Africa Tanzania, kuwa daraja katikati ya wakulima, serikali na wadau kuwasaidia kuinua uchumi wa mkulima mmoja mmoja.

Kwa sasa, alisema uhitaji wa miche mipya ya kahawa umekuwa mkubwa kutokana na faida inayopatikana sambamba na kuongezeka kwa uzalishaji kulinganisha na ilivyokuwa awali. "Licha ya manufaa mbalimbali tunayoyaona kwa wakulima wetu, bado wanakabiliwa na tatizo la kupanda kwa pembejeo za kilimo ambazo zinachangia kukwamisha jitihada za uzalishaji," alisema.

Alisema licha ya kupanda kwa pembejeo za kilimo husani mbolea kutoka Sh. 69,000 kwa mfuko mmoja hadi 120,000 pia upatikanaji wake umekuwa mgumu, hivyo akaomba serikali kuliangalia kwa jicho la karibu suala hilo.

Akifungua kikao hicho, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Donald Bombo, alisema Cafe Africa Tanzania kupitia mradi wa CODE P hadi kufikia Mei, mwaka huu, imewafikia wakulima 11,999 wakiwamo wanawake 3,719 na kwamba katika kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2021. Lengo lilikuwa kuwafikia wakulima 12,000.

## Wanaswa tuhuma za wizi, kuvunja nyumba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limefanya msako na doria kwa siku nne na kuwakamata watuhumiwa saba kwa makosa ya kuvunja nyumba usiku na kuiba, kupatikana na pombe moshi (gongo) na mali za wizi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alisema msako na doria hiyo vilifanyika Mei 20 hadi juzi.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Meston Mwakayamba (23) mkazi wa Mapelele, aliyekamatwa Jumapili iliyopita saa 3:00 asubuhi akiwa na TV mbili za inchi 24, jiko la gesi na redio aina ya Aborder Subwoofer. Alisema mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani.

Mwingine ni Penina Maganga mkazi wa kitongoji cha Kilambo wilayani Kyela ambaye alikamatwa Mei 21 majira ya saa 3:00 usiku akiwa na lita 10 za gongo ambayo alihifadhi kwenye chupa tatu za maji ya kunywa na dumu la lita tano.

Pia alisema jeshi hilo lilimkamata Eliya Yohana (35), mkazi wa Rujewa kwa tuhuma za wizi wa mifugo baada ya kukutwa na kondoo wawili majike kwenye machinjio ya Rujewa ambako aliwapeleka kwa ajili ya kuchinjwa.

Alisema kondoo hao walikuwa na thamani ya Sh. 160,000 na kwamba mtuhumiwa alipohojiwa alikiri kuhusika na tukio hilo kueleza kuwa aliwaiba nyumbani kwa Ngapunde Masingisa Mei 20.

Mtuhumiwa mwingine, kwa mujibu wa Kamanda Matei ni Emmanuel John (28) mkazi wa Sumbawanga aliyekamatwa katika eneo la stendi ya Rujewa akiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 202 CYR aina ya Kinglion yenye rangi nyekundu.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya kuonekana mwenye shaka hali iliyowalazimu polisi kuhoji nyaraka za pikipiki hiyo na kushindwa kutoa na kukiri kuwa hana kadi na kwamba aliinunua kwa Sh. 350,000 wilayani Chunya kwa mtu anayemtambua kwa jina moja la Edward.

Kamanda Matei alisema upelelezi wa shauri hili unaendelea ikiwa ni pamoja na msako wa kumpata mtuhumiwa mwingine ambaye ni muuzaji wa pikipiki kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Watuhumiwa wengine ni Asumwisye Mwalungwe (35) na Ayubu Mashamwaisemba (30) wote wakazi wa Kijiji cha Lusungo wilayani Kyela ambao walikamatwa wakiwa na gongo lita 100 zikiwa zimebebwa kwenye baiskeli ndani ya madumu matano ya lita 20.

Mtuhumiwa mwingine alimtaja kuwa ni Abraham Mwakambele (25), mkazi wa Ilemi aliyekamatwa na pombe aina mbalimbali zilizopigwa marufuku nchini zikiwamo Fighter katoni 30, Win 12, Ice Dry London Gin chupa 72, Jambo Gin chupa sita, Zikomo chupa 29, A One chupa moja, Power 35 na Hot Short chupa tano.





# Kilimo cha mwani chawakomboa wakulima

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

LICHA ya kilimo cha mwani kukabiliwa na changamoto nyingi, hali ni tofauti kwa wakulima wa zao hilo katika kijiji cha Tumbe, Kaskazni Pemba.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo wakizungumza na waandishi wa habari waliofika kijijini hapo katika ziara maalum iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), wakulima hao walisema kilimo hicho ni mkombozi kwao.

Fatma Omar ni miongoni mwa wakulima hao, alisema kilimo cha mwani kimemtoa kutoka katika dimbwi la umaskini na sasa ana uhakika wa kupata kipato cha kujikimu kimaisha.

"Kilimo cha mwani ni mkombozi kwangu, napata chakula na kugharamia elimu kwa watoto wangu kwa kilimo hiki," alisema.

Mkulima mwingine Fatma Machano Ali, alisema kilimo hicho kimemwezesha kununua charahani ambayo anaitumia kumwingizia kipato cha ziada, kusaidia mahitaji ya nyumbani na kununua vitu vingine vya thamani.

"Kwa sasa sihitaji tena msaada wa wazee kwa mahitaji madogo ambayo nayamudu, lakini nasaidia familia yangu inapopungukiwa kipato," alisema.

Vile vile, alisema ingawa kilimo hicho kimewanufaisha kiuchumi, kina changamoto nyingi ambazo zimesababisha baadhi ya wananchi wa kijiji hicho kuachana nacho.

Pia mkulima Mariyam Said, alisema kutokana na ugumu wa kilimo hicho, bei ya Sh. 600 kwa kilo ya mwani ni ndogo, serikali na wanunuzi wafikirie kuiongeza.

"Pia, hatuna vifaa vya kisasa vya kukausha mwani, tunalazimika kuanika chini hali inayosababisha mwani kukosa ubora na kuharibika wakati wa msimu wa mvua," alisema.

Naye Asha Khamis Sultan, Ofisa Kilimo cha mwani kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu, alisema serikali inachukua hatua kuboresha kilimo hicho.

Alisema miongoni mwa juhudi hizo ni kuwapatia wakulima boti 500 kupitia fedha za ahueni za Covid-19 ambazo zitawezesha wakulima kulima katika kina kirefu.

Aidha, alisema serikali kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), imeanza kununua mwani na bei inatofautiana kulingana na aina ya mwani.

"Kwa mwani mwembamba (spinosum) wakulima wanauza Sh.700 na mwani mnene (cottonii) Sh.1,800. Pia tunawahamasisha kuongeza thamani badala ya kuuza ghafi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema chama hicho kinaendelea kuwejengea uwezo waandishi wa habari ili kuwa na ujuzi wa kuandika habari za mazingira zenye tija kwa Watanzania wakiwamo wakulima wa mwani.

Kwa upande wake, Basco Huruma Kimambo, ni mfanyakazi wa kampuni ya Seaweed Corporation ambayo ni moja ya kampuni za mwanzo za ununuzi mwani, alisema Zanzibar ni moja ya nchi zinazozalisha zao hilo kwa wingi, lakini hautumiki kwa matumizi ya ndani badala yake unasafirishwa na bei inapangwa na walaji.

Hata hivyo, alisema usafirishaji wa mwani uliathiriwa vibaya na ugonjwa wa Covid-19 na kusababisha soko la ndani kuathirika.

Kampuni hiyo ina mwani wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni moja unaosubiri kusafirishwa.

Kilimo cha mwani Zanzibar kilianza mwaka 1989 na hadi sasa kuna wakulima zaidi ya 36,000 wengi wao wakiwa wanawake na asilimia 70 wako katika Wilaya ya Micheweni ikiwamo Kijiji cha Tumbe.

## Serikali kukinusuru kisiwa cha Mnemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeanza kutekeleza mikakati ya kimazingira katika kukinusuru kisiwa cha Mnemba ambacho kipo katika tishio la hatari ya kutoweka kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Sulubu Kidongo, aliyetaka kujua kama serikali inafahamu hatari inayokikabili kisiwa cha Mnemba kilichoko Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja kutokana na kasi ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema kisiwa cha Mnemba kipo katika mfumo wa fungu lenye mchanga mwingi na kutokana na kasi ya maji ya baharini yamekuwa yakichukua mchanga huo na kusababisha hatari ya kisiwa hicho kutoweka.

Kadhalika alisema wizara imefanya mazungumzo na mmiliki wa kisiwa hicho aliyekodishwa kuhusu njia za kukiokoa kisiwa katika tishio la kutoweka.

Alisema serikali imeanza kuchukua juhudi za kujenga ukuta kwa ajili ya kuyanusuru maeneo yaliyoathirika na tishio la mazingira na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Aidha, serikali imeanza kuotesha miti pembezoni mwa ufukwe wa bahari kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kwa baadhi ya maeneo ambayo yameathirika vibaya.



Mkulima wa mwani, Fatma Omar kutoka kijiji cha Tumbe, Kaskazini Pemba, akionyesha kwa waandishi wa habari jinsi ya kuandaa mwani kwa ajili ya kuupanda, walipofanya ziara ya mafunzo kwa wakulima wa zao hilo, iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wananchi Pemba walilia meli ya uhakika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka serikali kununua meli ya uhakika itakayotowa huduma za usafirishaji abiria kwa wananchi wa kisiwa hicho na maeneo mengine kwa lengo la kukuza na kuimarisha shughuli zao za kiuchumi na kibiashara.

Wakichangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022-2023, katika kikao cha baraza hilo, Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame, alisema wananchi wa kisiwa cha Pemba miongoni mwa shughuli zao kubwa za kukuza uchumi na maendeleo ni safari za kibiashara kati ya Unguja, Tanga pamoja na Dar es Salaam ambako husafirisha bidhaa mbalimbali.

Alisema kwa sasa wananchi wa Pemba wanakabiliwa na tatizo la usafiri kufuatilia meli za serikali kusitisha safari zake na huduma za usafirishaji kufanywa na vyombo vya usafiri vya watu binafsi.

"Mheshimiwa kilio kikubwa cha wananchi wa Pemba kwa sasa wanahitaji meli itakayotowa huduma za usafirishaji wa abiria na mali zao ambayo inamilikiwa na serikali," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, Said Salim, alisema kukosekana kwa meli ya uhakika ya usafiri kwa wananchi wa Pemba ni changamoto kubwa inayorudisha nyuma juhudi za wananchi hao katika kujiimarisha kiuchumi na maendeleo ya kibiashara.

Alisema hivi sasa zipo meli zinazofanya safari katika kisiwa cha Pemba, lakini kutokana na changamoto mbalimbali inayojitokeza ikiwamo kuongezeka kwa gharama za usafirishaji upo uwezekano mkubwa wa wamiliki wa meli hizo kuongeza bei.

"Wananchi wa Pemba wanahitaji huduma za usafiri wa meli kila siku, lakini zipo dalili kwamba huduma hizo zinaweza kupungua hatua ambayo itasababisha usumbufu mkubwa," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake Mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Khamis Hamad, aliitaka serikali kukamilisha mchakato wa ununuzi wa meli itakayokuwa na sifa na uwezo wa kutoa huduma za usafirishaji.

Aidha, aliitaka Wizara ya Ujenzi kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Wete ambayo ni kiungo muhimu cha kuunganisha wananchi wa mikoa miwili ya kisiwa cha Pemba.

"Mheshimiwa Naibu Spika tunahitaji ujenzi wa Bandari ya Wete Pemba ambayo tunaamini itasaidia kuharakisha huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo na kuongeza kasi ya biashara kwa wananchi wake," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepongeza mikakati ya Wizara ya Ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete ambayo kwa muda mrefu ujenzi wake ulikwama kwa sababu mbalimbali.

"Nimefurahishwa na ahadi za wizara ya ujenzi mawasiliano na usafirishaji wa ujenzi wa barabara za vijijini ikiwamo ya Wete hadi Chake Cahake ambayo matumaini yetu makubwa inakwenda kufunguwa mikoa miwili ya Pemba katika mikakati ya uwekezaji," alisema Hassan Hamad, Mwakilishi wa Jimbo la Kojani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO TANGAZO

**IRIBA COMPANY LTD** ni Kampuni iliyosajiliwa kwa namba **154149155** kwa kufanya kazi zifuatazo;

1. Contractors zote
2. General supply

Inauzwa kwa mtu yeyote ambaye yupo tayari.Kampuni hiyo haidaiwi na serikali wala taasisi yoyote ile na imekamilika kwa vibali vyote vya serikali .

**Kwa mawasiliano ;**
**Whatsup: 0764955454 / 0764178508.**
Email:**Iribacompanyltd@gmail.com**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ADAMU HAJI SULEIMAN anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya ISUZU yenye namba za usajili T 295 APS. Lenye chases namba 1075526. KADI namba. 896247. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. **Taarifa ya polisi RB. Namba IRI/IRI/RB/157122/2022.**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**JOHAIVEN JOHANSEN KAJUNA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASIPOTI YA KUSAFIRIA (HATI) YENYE NAMBA **TAE 138460** ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI NCHINI TANZANIA MWAKA 2018.

KWA YEYOTE ATAKAYE IOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI: KAH/RB/545/2022**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **CITI BANK TANZANIA , Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara Majenereta (GENERATORS) yaliyoko kwenye jeduali, mnada utafanyika Tarehe 03/06/2022, katika yard yetu iliyopo Tabata Kimanga kuanzia saa mbili asubuhi,

| SERIAL NO. | MODEL | CAPACITY |
|---|---|---|
| A09KAWZ200 | CUMMINS-C550D5 | KVA 550 |
| OLY00000KR P801998 | OLYMPIA-GEPX110 | KVA 110 |

**MASHART YA MNADA**

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi,Genereta linauzwa kama liilivyo, Ukaguzi utaanza **Tarehe 27/05/2022**

**Mawasiliano piga: -**
**0715-683777/0786-139363**
**info@sepcoauctioneering.co.tz**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NELSON MKWERU NG'OKOROME** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **ORDINARY DIPLOMA IN COMPUTER ENGINEERING** chenye usajili namba 201411018 ,kilichotolewa na **MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/89553/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ESTER BUU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.1013/0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Chief Dodo mwaka 2007. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **MAN/BAB/RB/199739/2022.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676***

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Majosho mapya 500 kujengwa nchini

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema inapanga kujenga majosho mapya 500 nchini kwa ajili ya mifugo pia imeanza kutenga maeneo na kuwekeza nguvu kwenye malisho.

Kauli ilitolewa na Waziri wa Mifugo, Mashimba Ndaki wakati wa hafla iliyoandaliwa na taasisi inayojihusisha na masuala ya kilimo na ufugaji ya AgResult ya kuwazawadia wauzaji bora wa pembejeo kutoka mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Iringa.

Akizungumza baada ya hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Waziri Ndaki alisema katika kuunga juhudi za sekta binafsi kwenye sekta ya kilimo na ufugaji, serikali ilianza kujenga majosho 168 mwaka huu na tayari wametenga fedha nyingine kwa ajili ya ujenzi wa majosho mapya 500.

"Serikali inatambua juhudi za sekta binafsi kama taasisi hii ya AgResult katika kuinua sekta hii, nasi tunaungana nao na tumeanza kuwekeza nguvu kwenye maeneo mbalimbali ya mifugo," alisema Ndaki.

Alisema majosho hayo yakikamilika yatafanya idadi ya majosho yaliyojengwa kwenye kipindi cha miaka miwili kufika 668.

Vile vile, alisema serikali inatambua umuhimu wa shindano la AgResult la kutoa zawadi kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo na mifugo kwa wauzaji wadogo wadogo.

"Serikali inatambua Mradi wa AgResults, kwa jinsi unavyochangia katika utekelezaji wa mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo Tanzania. Hii inatupa imani kwamba kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, tunaweza kutatua changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya mifugo nchini Tanzania," alisema Ndaki.

Kwa upande wake Rodrigo Ortiz, kutoka Sekretarieti ya AgResults, alieleza kuwa mradi umejikita kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kupitia ubunifu wa mpango wa kutoa motisha ya zawadi ya fedha ili kushirikisha sekta binafsi kwa lengo la kunufaisha mnyororo mzima wa thamani.

"Awamu ya pili umepata mafanikio kutokana na majaribio na ubunifu katika mauzo ya awamu ya kwanza. Tumefurahishwa sana na mafanikio ya washindani na jinsi wanavyoendelea kuwekeza muda na rasilimali, kubuni mbinu mpya za kuwafikia wakulima na kuwawezesha kupata pembejeo muhimu na huduma za ugani," alisema Ortiz.

Msimamizi wa mradi huo, Neema Mrema, alisema AgResult inatambua juhudi za kila mshindani kwenye tuzo hizo.

# PM aiagiza Wizara Nishati wigo matumizi ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa ameitaka Wizara ya Nishati kuendelea kupanua wigo wa matumizi ya nishati ya gesi asilia ili kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na ukataji wa misitu nchini.

Alisema hayo jana wakati alipotembelea maonesho ya Majukumu ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.



Alisema wizara iendelee kupanua wigo wa kufikia Watanzania wengi zaidi katika mikoa mbalimbali nchini. "Tupanue wigo wa huduma hii iwafikie watu, tumeanza na Dar es Salaam, tuje kwenye majiji, manispaa zetu na hata hapa Dodoma tuwe na tawi na kazi hii iendelee"

Aidha, Waziri Mkuu amewataka watendaji wote katika sekta ya nishati kuhakikisha wanasimamia upatikanaji wa nishati ya umeme na nishati nyingine ikiwamo mafuta ili kuendelea kuiwezesha nchi kupata fursa ya kuendelea kukua kiuchumi.

"Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imeitaka serikali kuhakikisha upatikanaji wa umeme katika vyanzo vyetu unaimarishwa, kuendelezwa na kuhakikisha usambazaji wa umeme unawafikia wananchi mpaka vijijini ili kila Mtanzania anufaike kwa kupata nishati hiyo," alisema.

Maonesho hayo ya siku tatu yaliyoanza Mei 23, 2022 katika viwanja vya Bunge yalikuwa na lengo la kuwawezesha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuuliza maswali kuhusu huduma zinazotolewa na Wizara ya Nishati na taasisi zake.



Kaimu Mtendaji Kata ya Luhunga, Mussa Alphonce (kulia), akikabidhi nguruwe kwa wawakilishi wa vijana 100 kutoka mazingira magumu katika kata tatu za Ihanu, Mdabulo na Luhunga, Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, waliotolewa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wanufaika na msaada wa nguruwe kujikwamua na hali ngumu kimaisha

**Na Francis Godwin,** IRINGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa kwa kushirikiana na mradi wa Youth Angecy Mufindi (YAM) imetumia zaidi ya Sh. milioni 14 kuwapatia msaada wa nguruwe vijana 100 wanaotoka katika mazingira magumu kwenye kata za Luhunga, Ihanu na Mdabulo.

Akikabidhi jana msaada huo, Meneja Miradi ya YAM, Zilipa Mgeni, alisema taasisi hiyo imekuwa ikitekeleza mradi wa kuwasaidia vijana kwenye vijiji 16 vya kata hizi walengwa wakuu wakiwa vijana wanaotoka katika mazingira magumu, wakiwamo waliokatisha masomo kutokana na changamoto mbalimbali za kimaisha.

Mgeni alisema vijana hao kabla ya kukabidhiwa nguruwe hao ambao ni mtaji kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi, waliwapatia elimu ya ujasiriamali na elimu ya afya ya akili ili kujitambua na kuondokana na maisha ya kushinda vijiweni bila kazi kutokana na kukata tamaa ya maisha.

Alisema kupitia mradi huo wa miaka minne ulioanza mwaka jana, vijana hao wataendelea kunufaika na mradi huo unaotekelezwa kwa ushirikiano mkubwa na serikali katika wilaya.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi chini ya mradi wa Foxes Community and Wildlife Conservation (FCWC) na YAM kupitia ufadhili wa Finland, utatekelezwa kwenye kata hizo na utawanufaisha vijana na watoto wanaotoka katika familia duni wapatao 770.

Mgeni alisema vijana hao ambao wamepatiwa nguruwe kama mtaji, ni sehemu ya vijana 770 ambao watanufaika na mradi huo kwa kipindi chote cha miaka minne ya utekelezaji.

Alisema kila kijana ambaye ni mnufaika na mradi huo, amepatiwa nguruwe wawili, dume na jike, pamoja na chakula cha mwezi mmoja wa mwanzo.

Akizungumza kwa niaba ya wanufaika wa mradi huo, Felix Kitinusa alisema msaada huo ni ukombozi mkubwa kwake kwa kuwa muda mrefu alikuwa akitamani kuwa mfugaji wa nguruwe, lakini kikwazo kikubwa kilikuwa elimu na mtaji wa kuendeshea shughuli hiyo.

Kaimu Mtendaji wa Kata ya Luhunga, Mussa Alphonce, alipongeza mradi wa YAM na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa kuwafikia vijana hao wenye mazingira magumu na kuwa kupitia msaada huo, anaamini vijana wengi waliokuwa wakishinda vijiweni sasa watajikita katika shughuli za uzalishaji mali.

# SABABU KOCHA MBEYA CITY NUSURA KUCHEZEA KICHAPO

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

KOCHA Mkuu wa timu ya Mbeya City, Mathias Lule, amenusurika kuchezea kichapo kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo baada Jeshi la Polisi kuingilia kati na kulazimika kumtoa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa juzi chini ya ulinzi mkali.

Tukio hilo lilitokea juzi baada ya mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union kumalizika na mashabiki hao wa Mbeya City kukerwa na matokeo ya timu yao kukubali kipigo cha bao 1-0 uwanjani hapo.

Baadhi ya mashabiki waliokuwa wameshika mawe walikuwa wakitaka 'kumpopoa' kocha huyo wakimtuhumu kuwa na ugomvi na baadhi ya wachezaji jambo ambalo linasababisha matokeo mabaya kwa timu hiyo.

Aidha, mashabiki hao walikuwa wakimtuhumu kwa kutowatumia wachezaji muhimu kama mshambuliaji Paul Nonga na kiungo mshambuliaji, Peter Mapunda ambao ni miongoni mwa wachezaji wanaodaiwa kutoelewana na kocha huyo.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa mashabiki wa timu hiyo, Mashaka Mwakajwanga, alidai kuwa kufanya vibaya kwa timu hiyo, kunahusishwa na mambo mengi moja likiwa ni kocha huyo kudaiwa kuingia mkataba wa kisiri na klabu nyingine ya nchi jirani ya Malawi kabla ya hata ya msimu kumalizika, lakini kuwapo kwa uhasama baina yake na wachezaji.

"Tunahujumiwa na kocha wetu haiwezekani kwenye kikosi anashindwa kuwaweka wachezaji kama Paul Nonga na Peter Mapunda ambao kwa mchezo wa leo wangeipatia matokeo mazuri timu yetu, bifu lake na wachezaji linaigharimu klabu yetu ambayo kwenye mzunguko wa kwanza ilifanya vizuri," alisema Mwakajwanga.

Baraka Mwangisi alisema kwa matokeo ya Mbeya City kukubali vichapo mara tatu mfululizo kunaiweka kwenye hali mbaya katika msimamo wa Ligi kuu ya NBC.

Alisema kwa mwenendo huo Kocha Lule anapaswa kujitathmini kama anafaa kuendelea kukinoa kikosi hicho au kuondoka kutokana na matokeo mabaya ambayo yanawaumiza mashabiki na kuhisi ni hujuma wanafanyiwa.

Akizungumzia mchezo huo, Kocha Mbeya City, Lule alisema jukumu lake ni kuitengeneza timu kiufundi na si kusikiliza maneno ya mashabiki huku akisisitiza kuwa timu yake ilitengeneza nafasi nyingi, lakini ikashindwa kuzitumia.

Alisema pamoja na matokeo kutokuwa mazuri, lakini bado timu hiyo ina nafasi ya kufanya vizuri kutokana na kubakiwa na michezo minne ambayo miwili itacheza katika uwanja wa nyumbani na mingine ugenini.

"Kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuitengeneza timu, tumetengeneza nafasi nyingi tukashindwa kuzitumia, lakini wenzetu wametengeneza nafasi moja na wakaitumia vizuri, tutaendelea kurekebisha makosa katika michezo iliyobaki ili tupate mafanikio," alisema Lule.

Kwa upande wa Kocha wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema pamoja na kupata ushindi, lakini walipata wakati mgumu kutokana na kucheza mchezo huo mchana wakati wa jua kali.

Hata hivyo, alisema matokeo waliyoyapata kwenye mchezo huo ni kipimo kizuri cha timu yake kuelekea mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya 'Wanalambalamba', Azam FC.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na kupata matokeo ambayo yamewaweka katika nafasi nzuri.

Matokeo hayo yainafanya Coastal Union kukaa katika nafasi sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 34 wakati Mbeya City inabaki na pointi zake 32 katika nafasi ya nane, timu hizo kila moja ikiwa imeshuka dimbani mara 26.




Nahodha wa Keko Furniture FC, Rahim Kiana (kushoto), akipokea msaada wa jezi kwa niaba ya timu yake, kutoka kwa Meneja Masoko wa 10bet Tanzania, George Abdulrahaman, wakati wa makabidhiano rasmi yaliyofanyika katika eneo la Keko, Dar es Salaam jana. Kampuni hiyo, ilitoa vifaa vya michezo kwa timu 14 tofauti zinazoshiriki Ndondo Cup. **MPIGAPICHA WETU**

# 10bet yazipiga jeki timu 14 za Ndondo Cup

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI inayokua kwa kasi ya michezo ya Kubashiri Tanzania, 10bet, imetoa msaada wa vifaa vya soka kwa timu 14 zinazoshiriki michuano ya Ndondo Cup mwaka 2022 kama sehemu ya mpango wake unaoendelea kusaidia michezo ya ndani katika nchi wanazofanyia kazi.

Kenan van Damme, Meneja wa 10bet Tanzania, alizitaja timu zilizopokea jezi zao mpya kuwa ni Moro Warriors FC, Ujugu FC, Manzese Warriors FC, Keko Furniture FC, Kisa FC, Chuganism FC, Wagaigai FC, Planet FC, Vigezo Combine FC, Mshikamo City FC, Changombe Youth FC, Kigogo Fresh FC, Jaguar FC na Jet Lumo FC.

"Tunafuraha sana kupokea vifaa vya soka kutoka kwa 10bet, kupata shukrani na usaidizi kama huo kunatia moyo, haswa kwa timu za ndani ambazo hazipati usaidizi mara kwa mara. Inatia moyo kwamba umakini zaidi unatolewa kwa mashindano ya ndani ya kandanda yenye matarajio, na tunatazamia michezo iliyo mbele yetu," alisema Nahodha wa Keko Furniture FC, Rahim Kiana.

10bet ilizinduliwa hapa nchini Agosti 2021 kama sehemu ya mkakati wa kampuni hiyo kujitanua barani Afrika na sasa iko katika nchi tano tangu kuanzishwa kwake barani. Kampuni hiyo imepanga kuongeza soko la sita kwenye orodha yake kabla ya mwishoni mwa mwaka huu.

"Tunapenda sana michezo na kama raia tunaowajibika, tunaelewa athari za michezo ya ndani kwa jamii. Tumejitolea kuendelea kusaidia jamii zetu za ndani kupitia mipango endelevu ya michezo," alisema Meneja wa 10bet Tanzania, Van Damme.

10bet ilianza kuwekeza katika michezo ya Kiafrika kwa kusaini mikataba mikuu ya udhamini na klabu sita za daraja la juu la soka: Dodoma Jiji FC (Tanzania), Talanta FC (Kenya), Red Arrows (Zambia), Aduana Stars (Ghana), Enyimba (Nigeria) na Daring Club Motema Pembe (DRC). Aidha, 10bet inatoa zaidi ya masoko 2,000 ya kubashiri na zaidi ya matukio 25,000 ya moja kwa moja kwa mwezi, wateja na wadau nchini sasa wanaweza kuweka dau kwenye michezo, Jackpot, na michezo ya mtandaoni kupitia simu ya mkononi, USSD, na Programu mpya ya Android.

Malipo yao ya papo hapo yamethibitika kuwa mojawapo ambayo ni bora zaidi sokoni na wateja wanaweza kujaza akaunti zao kupitia M-Pesa, Airtel Money na Tigo Pesa.

# Katwila, Ihefu FC kujadili mkataba

Na Saada Akida

UONGOZI wa Mabingwa wa Championship 2022, Ihefu FC, umeweka wazi kuwa wanahitaji kumwongezea mkataba Kocha Mkuu wao, Zuberi Katwila, ili kuendelea kukinoa kikosi cha timu hiyo iliyorejea kwa mara nyingi Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ihefu FC wametawazwa kuwa Mabingwa wa Championship baada ya kumaliza ligi hiyo wakiwa na idadi kubwa ya mabao baada ya kufungana pointi 66 na DTB FC, ambayo imemaliza nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Ihefu FC, Zagalo Chalamila, alisema baada ya Katwila kukabidhi ripoti na tathmini ya kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara, wataanza mazungumzo ya kumwongezea mkataba baada ya ule wa awali kufikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu.

"Jambo la kuwapongeza wachezaji na benchi la ufundi kwa timu kurejea Ligi Kuu, kuhusu Kocha Katwila bado yupo katika mipango yetu na ndani ya hizi siku mbili tunakutana naye kwa ajili ya mazungumzo ya mkataba mpya kama ataridhia ataendelea kubaki katika timu yetu," alisema Chalamila.

# Warriors Queens yanusa ubingwa

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Warriors Queens imekaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar msimu huu baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya wapinzani wao wakuu ambao ni Mabingwa Wetetezi wa ligi hiyo, New Generation.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Mau B juzi, Stefania Gerad ndiye aliyeitanguliza Warriors katika dakika ya tatu kabla ya Hawa Ali kuifungia New Generation bao la kusawazisha dakika ya 37.

Kwa matokeo hayo, sasa Warriors imefisha alama 43 huku wapinzani wao wakiwa na pointi 40 na kila timu imebakisha michezo mitatu kabla ya msimu kumalizika.

Warriors Queens wameshinda michezo 14 katika ya 15 iliyocheza hadi sasa huku ikitoka sare mechi moja wakati wapinzani wao, New Generation wakishinda michezo 13, wakipoteza mmoja na sare moja.

Akizungumza na gazeti hili, nahodha wa Warriors Queens, Neema Machano, alisema licha ya kuwafunga Mabingwa Watetezi, New Generation, ambao ndio wapinzani wao wakubwa wanaoweza kubadilisha msimamo wa ligi hiyo, malengo yao ni kuhakikisha wanashinda mechi zilizobaki.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL NA OSIMHEN

ARSENAL wamefanya mazungumzo kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Napoli na timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, 23 na wanaendelea na jaribio la kumnyakua mshambuliaji, Gabriel Jesus, 25, kutoka Manchester City. ***(Goal)***

### SUAREZ KUMFUATA BECKHAM

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suarez, 35, huenda akahamia klabu ya Inter Miami ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MSL), baada ya kuachwa na Atletico Madrid. ***(Independent)***

### TUCHEL PAUNI MIL. 200

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel anatarajiwa kupata pauni milioni 200 za kutumia msimu huu wa majira ya joto huku uhamisho wa Todd Boehly ukikaribia kukamilika baada ya Ligi Kuu ya England kutangaza kuuzwa rasmi kwa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### RAPHINA AITAKA BARCA

WINGA wa Brazil, Raphinha, 25, amewaambia wakurugenzi wa Leeds United kwamba, anataka kuchezea Barcelona, ambao walitoa ofa ya pauni milioni 30 iliyokataliwa mapema mwaka huu. ***(Sport)***

### CAVANI ATAKIWA SERIE A

KLABU ya Salernitana inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A, "ingependelea kumsajili" mshambuliaji wa Manchester United anayeondoka, Edinson Cavani, 35, kwa mujibu wa rais wa Salernitana, Danilo Iervolino. ***(Manchester Evening News)***

### HAZARD HAONDOKI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Eden Hazard, 31, hana mpango wa kuondoka Real Madrid, na amesisitiza kuwa anataka sana "kuonyesha uwezo wake" baada ya miaka yake mitatu ya kukabiliwa na majeraha. ***(Goal)***

### SARR AWANIWA EVERTON

EVERTON na Crystal wanataka kumsajili winga wa Watford na Senegal, Ismaila Sarr, 24, lakini Newcastle wamesitisha azma yao ya kumsaka kiungo huyo. ***(Football Insider)***

### BALE AKATALIWA ATLETICO

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 32, alitolewa kwa Atletico Madrid kwa uhamisho huru, lakini walimkataa. Bale anatarajiwa kuondoka kwa wapinzani wa Atletico, Real Madrid katika majira haya ya joto. ***(Marca)***

### DUBRAVKA KUBAKI NEWCASTLE

GOLIKIPA wa Slovakia, Martin Dubravka, 33, anataka kubakia Newcastle, licha ya klabu hiyo kuhusishwa na kutaka kumnunua mlinda mlango wa Manchester United na England, Dean Henderson, 25 ama kipa wa Chelsea na Hispania, Kepa Arrizabalaga mwenye miaka 27. (***Chronicle***).

### NANE KUSAJILIWA CHELSEA

MLINZI wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde, 23, na kiungo wa kati wa RB Leipzig, Josko Gvardiol, 20, wako kwenye orodha ya wachezaji nane wanaotarajiwa kusajiliwa Chelsea msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KACHAGUA CITY MBELE YA PSG, MADRID

**Ameichagua kwa sababu ya mradi wa City, anacholipwa kinaweza kulipwa na klabu hizo...**

**MANCHESTER,** England

MTENDAJI Mkuu wa Manchester City Football Group, Ferran Soriano, amesema Erling Haaland angeweza kwenda popote, lakini alichagua kucheza chini ya Pep Guardiola hapo Manchester.

**Mshambuliaji huyo wa Norway alitua jijini Manchester Jumanne kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 51 kutoka Borussia Dortmund, baada ya kukamilisha vipimo vya afya yake.**

City ilishinda taji la Ligi Kuu England bila mshambuliaji msimu huu, huku Kevin De Bruyne, Raheem Sterling na Riyad Mahrez wakiwa wachezaji watatu waliovuka kizuizi na kufunga mabao 10.

Soriano anaamini kwamba, Haaland atabadilika na kustawi ndani ya City na licha ya jinsi kikosi cha Guardiola kilivyokabiliana na hitaji la mshambuliaji wa kati kama yeye msimu huu, bado anahitajika.

"Haaland ametuchagua kwa sababu tulimweleza mradi wetu," alisema Soriano akiiambia RAC 1.

"Tunachomlipa kinaweza kulipwa na PSG, (Manchester) United, Bayern (Munich) au Real Madrid. Tunaweka kipaumbele kwenye soka.

"Haaland atahitaji kipindi cha marekebisho na itabidi tuwe na subira, lakini atafanikiwa.

"Mtazamo wetu uko kwenye mpira wa miguu, kucheza vizuri na kushinda, badala ya wachezaji nyota, tulikuwa tunakosa mshambuliaji wa kati.

"Tulikuwa na mtu wa kuvutia kama (Sergio) Aguero. Tulimpoteza kwa sababu ya umri wake, na tumekuwa tukitafuta mbadala wake kwa zaidi ya mwaka mmoja na Haaland ni mmoja."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ROSENBORG
VERSUS
HAUGESUND
1 | 1.47
X | 4.38
2 | 5.97

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BENZEMA AKANA KUMWITA MBAPPE MSALITI MADRID

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amesisitiza kuwa haoni "kusalitiwa" na uamuzi wa Kylian Mbappe kuamua kubakia Paris Saint-Germain badala ya kujiunga naye Real Madrid.

Baada ya zaidi ya mwaka wa uvumi mkubwa, Mbappe hatimaye alithibitisha Jumamosi kwamba, alikuwa amesaini mkataba mpya wa miaka mitatu na PSG.

Ulikuwa uamuzi ambao wachache waliona unakuja kutokana na uhakika wa Madrid kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa angejiunga nao kwa uhamisho wa bure mwishoni mwa Juni.

Uamuzi wa Mbappe ulimkasirisha mkuu wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas, huku wengine waliohusishwa kwa karibu zaidi na Madrid wakisemekana kupigwa na butwaa.

Chapisho la Instagram la Benzema baadaye siku hiyo hiyo lilivutia umakini wa kipekee, alipoweka picha ya marehemu rapa Tupac Shakur ambayo alikuwa na watu wake wa karibu, ambao wanadaiwa kumsaliti na kuhusika na kifo chake mwaka 1996 alipouawa kwa kupigwa risasi.

Kwa mujibu wa gazeti la mjini Madrid la Marca, ambalo kwa ujumla linaonekana kuwa na uhusiano mkubwa na 'Los Blancos' hao, Benzema alikuwa muhimu katika kujaribu kumshawishi mchezaji mwenzake wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Mbappe ajiunge na klabu hiyo, ndiyo maana huenda alihisi kusalitiwa.

Lakini Benzema anasisitiza kwamba habari kama hizo ni za upuuzi.



## *Arteta: Saliba atacheza msimu ujao*

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesisitiza kuwa William Saliba atarejea hapo kwenye dimba la Emirates msimu ujao baada ya mwaka mmoja kule klabu ya Marseille.

Beki huyo wa kati ametumia msimu huu kwa mkopo katika klabu hiyo ya nchini Ufaransa, na ripoti zimedai kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anatarajia kubaki kwenye Ligue 1 kwa msimu mwingine.

Lakini Arteta amesema atamhitaji Saliba msimu wa 2022-23 wakati Arsenal wakikabiliana na majukumu ya Ligi ya Europa pamoja na Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, alisajiliwa na Arsenal kutoka Saint-Etienne Julai 2019, lakini mara moja akarudishwa kwa mkopo Les Verts, na baadaye akapelekwa kwa mkopo Nice na Marseille.

Saliba alikuwa na kiwango cha kuvutia Marseille, ambao walimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligue 1, na alichaguliwa kwenye kikosi bora cha ligi hiyo msimu huu.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# MIL. 32/- JACKPOT BONUS YA SPORTPESA ZAENDA KOROGWE

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, Leonard Patrick Ngaja, ameshinda Sh. 32,417,640 katika Jackpot Bonus ya SportPesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

**Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya hundi katika ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam, Leornard alisema alianza kucheza na kampuni hiyo miaka mitatu iliyopita.**

"Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2019 baada ya rafiki yangu kunifundisha kucheza," alisema Leornard ambaye ni mkulima na mjasiriamali.

"Kwa kweli namshukuru sana jamaa yangu Mosha, unajua wakati ule kabla sijaanza kucheza nilikuwa nawaona wao wanavyocheza na kushinda."

Alisema huwa anacheza Jackpot na michezo mingine kwa kutumia simu yake ya kitochi ama kiswaswadu, lakini mara nyingi anacheza Jackpot zaidi.

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Jackpot Bonus, alisema aliweka mkeka wake siku ya Ijumaa na baada ya hapo ilipofika Jumapili majira ya jioni alitizama mkeka wake na kukuta ameshapatia timu sita.

Anaendelea kusema baada ya hapo alitazama mara ya pili alikuta amepata jumla ya timu tisa. "Kusema ukweli niliingiwa na kitete, hivyo nilishindwa kufuatilia mechi moja baada ya nyingine hadi usiku nilipolala. Nilipoamka majira ya saa 10 usiku ndipo nilipoona meseji ya hongera umeshinda."

Leonard anawashauri Watanzania wasisite kucheza kwa wingi kwani Jackpot ya SportPesa ni ya uhakika na matokeo yake ni papo kwa hapo bila kuchelewa. "Nawaomba muitumie fursa hii kwani ndio njia ya uhakika kulamba mkwanja kama mimi". Alisema fedha alizoshinda atawekeza kwenye kununua gari aina ya Canter na nyingine kwenye biashara yake ya kilimo kwa kuongezea mtaji.

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza mshindi huyo na kuwaasa Watanzania kuendelea kuiamini na kucheza na SportPesa kwani wanaweza kushinda kama Leonard.

"Niwakumbushe tu Watanzania Jackpot kwa wiki hii ni 222,883,040. Endeleeni kucheza mshinde kama Leonard," alisema.




Mshindi wa Jackpot Bonus ya SportPesa, Leonard Ngaja, kutoka Korogwe mkoani Tanga, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 32,427,640 alizoshinda baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot mwishoni mwa wiki. Jackpot ya wiki hii ni Sh. 222,883,040. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mgunda auliza waliosema Coastal itashuka

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amewauliza walipo wale waliokuwa wakisema Coastal Union itashuka daraja.

Akizungumza juzi baada ya mechi hiyo kumalizika kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, alisema kuna watu waliodhani kuwa watashuka daraja, lakini wameendelea kupambana mpaka sasa hawawezi kukata tamaa hadi mwisho wa ligi.

"Mimi nadhani waulizwe wale waliosema sisi tunashuka, wako wapi? Haya ni mashindano na sisi tunashindana na haiwi mwisho mpaka iwe mwisho. Mechi ya leo ilikuwa muhimu kwa pande zote mbili ili kujiweka sawa, lakini Mungu ametusaidia tumepata pointi tatu, tunazidi kujipanga, tunasonga mbele," alisema kocha huyo.

Coastal Union ambayo kuna wakati ilikuwa inaburuza mkia na baadhi ya mashabiki wa soka kudhani itashuka daraja msimu huu, kwa sasa imepanda hadi nafasi ya sita, ikiwa na pointi 34, ikibakisha mechi nne tu kabla ya msimu huu kumalizika, huku ikionekana kuwa salama kwenye eneo la hatari mpaka sasa.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, iliyopoteza nyumbani, Matias Lule alisema wachezaji wake walicheza vema mechi hiyo kuliko iliyopita, lakini walifanya kosa moja la kizembe ambalo limetumiwa na wapinzani wao.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 26/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3707 | Varbergs Gif FK vs Tolo IF | 2.34 | 3.63 | 2.52 |
| 15:00 | 4049 | Eskilsminne IF vs Vastra Frolunda IF | 1.60 | 4.09 | 4.38 |
| 15:00 | 4408 | Skive IK vs FA 2000 | 1.95 | 3.31 | 3.50 |
| 15:00 | 4457 | Uraedd FK vs Vindbjart | 4.57 | 4.28 | 1.55 |
| 15:00 | 4473 | IFK Berga vs Nosaby IF | 1.40 | 4.59 | 6.05 |
| 15:00 | 4636 | Ariana FC vs Rappe Goif | 1.75 | 4.10 | 3.95 |
| 15:00 | 4984 | BK Astrio vs Savedalens IF | 1.62 | 4.49 | 3.85 |
| 15:00 | 5216 | FC Rosengaard vs Osterlen FF | 2.14 | 3.31 | 3.02 |
| 15:30 | 2899 | Napoli Youth vs Genoa Youth | 2.29 | 3.55 | 2.63 |
| 15:30 | 3224 | Umeaa FC vs Taby FK | 1.51 | 4.29 | 4.87 |
| 15:30 | 3762 | VV Noordwijk vs TEC | 1.82 | 3.51 | 3.75 |
| 16:00 | 1459 | Hammarby vs Malmo | 2.09 | 3.32 | 3.12 |
| 16:00 | 1675 | IFK Uppsala vs FC Gute | 1.93 | 4.18 | 2.91 |
| 16:00 | 2173 | Vasalunds IF vs Tegs SK | 1.09 | 7.98 | 17.52 |
| 16:00 | 2615 | Kungsangens IF vs Hudiksvalls FF | 3.89 | 4.47 | 1.61 |
| 16:00 | 3280 | Sandviks IK vs IF Algarna | 1.95 | 3.56 | 3.27 |
| 16:00 | 4036 | Nordvarmland FF vs IK Gauthiod | 3.36 | 3.79 | 1.86 |
| 16:00 | 4143 | Kvarnsvedens IK vs FC Jarfalla | 2.81 | 3.68 | 2.11 |
| 16:00 | 4860 | Odense vs Midtjylland | 3.91 | 3.52 | 1.79 |
| 17:00 | 1274 | Gefle IF vs Piteaa IF | 1.49 | 4.19 | 5.26 |
| 17:00 | 1492 | Gottne IF vs Ytterhogdals IK 1921 | 1.43 | 4.47 | 5.64 |
| 17:00 | 4228 | Aatvidaberg vs IK Oddevold | 4.78 | 4.00 | 1.56 |
| 17:00 | 4849 | Gais vs Oskarshamns Aik | 1.55 | 4.00 | 4.88 |
| 17:15 | 4452 | Baniyas vs Ittihad Kalba | 2.12 | 3.56 | 2.87 |
| 17:30 | 2475 | B71 Sandoy vs NSI Runavik II | 1.27 | 5.84 | 7.20 |
| 18:00 | 1308 | Paide Linnameeskond vs Flora II | 1.58 | 4.79 | 4.39 |
| 18:00 | 1733 | Skeid Fotball vs Sandnes Ulf | 2.58 | 3.45 | 2.37 |
| 18:00 | 3397 | Valerenga IF 2 vs Tromsdalen | 3.78 | 4.26 | 1.67 |
| 18:00 | 5202 | Falkenbergs vs BK Olympic | 1.76 | 3.69 | 3.84 |
| 18:00 | 5209 | US Monastir vs Esperance Tunis | 4.39 | 2.88 | 1.90 |
| 19:00 | 1111 | Red Star Belgrade vs Partizan | 2.10 | 3.01 | 3.44 |
| 19:00 | 2290 | Rosenborg vs Haugesund | 1.47 | 4.38 | 5.97 |
| 19:00 | 2495 | IK Start vs Raufoss | 1.40 | 4.67 | 5.83 |
| 19:00 | 2520 | Aasane Fotball vs Grorud IL | 2.12 | 3.50 | 2.92 |
| 19:00 | 2561 | Fredrikstad vs Kfum Oslo | 1.89 | 3.60 | 3.41 |
| 19:00 | 3415 | Stjordals-Blink vs Sogndal | 3.12 | 3.41 | 2.06 |
| 19:00 | 4186 | FC Schaffhausen vs FC Luzern | 2.93 | 3.48 | 2.24 |
| 19:00 | 5534 | Mjondalen vs Ranheim | 1.70 | 3.65 | 4.19 |
| 19:00 | 5588 | Kongsvinger IL vs Brann | 4.38 | 3.84 | 1.64 |
| 19:00 | 5597 | Bryne vs Stabaek | 3.74 | 3.65 | 1.79 |
| 19:30 | 4980 | Al Masry Club vs National Bank | 2.41 | 3.13 | 2.94 |
| 20:00 | 3429 | Emirates Club vs Ajman Club | 4.85 | 4.46 | 1.49 |
| 20:00 | 5494 | HNK Rijeka vs Hajduk Split | 4.19 | 3.99 | 1.64 |
| 20:00 | 5583 | AJ Auxerre vs St Etienne | 2.42 | 3.18 | 2.88 |
| 20:45 | 1476 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 21:00 | 2906 | Vitesse Arnhem vs AZ Alkmaar | 2.88 | 3.37 | 2.29 |
| 21:00 | 4458 | Sarpsborg vs Molde | 2.68 | 3.47 | 2.42 |
| 21:30 | 4329 | Monza vs Pisa | 1.98 | 3.21 | 3.81 |
| 21:45 | 4694 | Arka Gdynia vs Chrobry Glogow | 1.73 | 3.51 | 4.19 |
| 22:00 | 3313 | Pyramids vs Coca Cola | 2.07 | 3.19 | 3.59 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Mei 26, 2022

Nipashe




## Arteta: Saliba atacheza msimu ujao

UKURASA 22

**CHUPUCHUPU!...**



Kocha wa timu ya Mbeya City, Mathias Lule, akipanda kwenye gari chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi baada ya mashabiki wa timu hiyo kutaka 'kumpopoa' mawe kutokana na matokeo mabaya dhidi ya Coastal Union iliyowachapa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, huku pia wakidai anaihujumu timu yao. **Habari kamili Uk.20. PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# SIMBA NA USAJILI WA KUTISHA MSIMU UJAO

## Mkakati kabambe waanza, huku Chama, Manula tayari kuivaa Yanga...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewaahidi wanachama na mashabiki wake kuwa itafanya usajili mkubwa kwa ajili ya msimu ujao kwenye michuano mbalimbali, ikiwamo Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ikitaka kwanza imalize msimu huu vizuri kwa kutwaa Kombe la FA.

**Simba itamenyana na Yanga katika mechi ya robo fainali itakayopigwa Jumamosi katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.**

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amekiri ni kweli kwa sasa klabu ipo kwenye mawindo ya usajili wa wachezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi, ingawa hakuwataja nyota wanaowawinda.

"Kwa kifupi ni kwamba tupo kwenye mawindo makubwa ya usajili, ukiangalia kikosi chetu msimu huu hatujakuwa na mwenendo wa kuridhisha na kupendeza, hatujakuwa na matokeo ambayo tunayataka na kuyapenda sisi Wanasimba. Kwenye mpira kama hupati matokeo unayoyakusudia basi unarejea kufanya usajili babu kubwa ili utimize malengo na ndiyo maana wachezaji wananunuliwa na kuuzwa.

"Kwa sasa wakati mipango hiyo inaendelea hawa tuliokuwa nao wanaendelea na tunajitahidi kupambana ili kumaliza msimu vizuri, na jinsi ya kuumaliza vizuri ni kuchukua Kombe la FA kwanza, baada ya hapo ndiyo tunakwenda kukaa kwenye meza kuangalia masuala ya kumalizia usajili," alisema Meneja Habari huyo.

Licha ya kwamba hakuwataja wachezaji wanaowanyemelea, tetesi zinawataja wachezaji ambao wako kwenye mazungumzo nao ni Victorien Adebayor wa US Gendamarie ya Niger, Moses Phiri wa Zanaco ya Zambia, Kwame Peprah raia wa Ghana anayechezea klabu ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, Luis Miquissone anayerejea kwa mkopo kutoka Al Ahly ya Misri, Cesar Manzoki raia wa nchi mbili, Congo DR na Afrika ya Kati, straika anayeichezea Vipers ya Uganda na mfungaji bora msimu huu, Soze Zemanga wa TP Mazembe, Idumba Fasika, beki wa kati anayeichezea Cape Town City ya Afrika Kusini pamoja na beki Mnyarwanda Thierry Manzi anayekipiga FAR Rabat ya Morocco.

Simba inatarajia kufanya usajili mkubwa baada ya kumalizika kwa msimu kutokana na kutofikia malengo msimu huu, ikionekana kupoteza ubingwa wa Ligi Kuu iliyouhodhi kwa misimu minne, kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kushindwa kutinga hatua ya makundi, ikiangukia makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini ikashindwa kufikia malengo yake ya kufika nusu fainali.

Kuhusu mechi ya Jumamosi, Ahmed alisema kutwaa Kombe la ASFC itakuwa faraja kwa Wanasimba, lakini kuifunga Yanga itakuwa jambo bora litakalowafanya kumaliza msimu kwa furaha.

Alisema kikosi chao kinaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na wachezaji ambao walikuwa majeruhi, Clatous Chama na Aishi Manula na wote wanaweza kuwa sehemu ya mchezo Jumamosi.

"Aishi Manula aliumia vidole viwili kabla ya mchezo wetu dhidi ya Geita Gold, lakini anaendelea vizuri na anafanya mazoezi ya kuchezea mpira na wachezaji wa ndani, kwa matibabu anayopata tunatarajia atakuwa fiti kabla ya mchezo.

"Kapombe naye anaendelea vizuri pamoja na Chama, ambaye alianza mazoezi mepesi Jumatatu na wote tunatarajia watakuwa tayari kwa mchezo wa Jumamosi," alisema huku akiwataka Wanasimba kujitokeza kwa wiki katika mchezo huo.

# Yanga: Waje tu, sisi tupo tayari

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Klabu ya Yanga, Cedrick Kaze (pichani chini), amesema pamoja na kuendelea kuinoa timu yao kuelekea mchezo wa nusu fainali wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), Jumamosi dhidi ya Simba, wapo tayari kwa kipute hicho kitakachopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na mwandishi wetu jana moja kwa moja kutoka Shinyanga walipoweka kambi kwa ajili ya mechi hiyo ambayo mshindi atakutana na timu itakayoshinda nusu fainali ya pili kati ya Azam FC na Coastal Union, alisema wameamua kujificha huko ili kuepuka usumbufu kwa wachezaji wao.

"Tunashukuru tunaendelea vizuri, wachezaji wapo tayari kukutana na timu ya Simba, tunafahamu mchezo utakuwa mgumu, lakini na sisi tumejipanga kuhakikisha tunashinda," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema lengo la kujificha Shinyanga ni kuwapa mazoezi vilivyo wachezaji wao ili wasipoteze mchezo wao huo, lakini kupata utulivu zaidi.

Alisema kutokana na mazoezi wanayowapa, wanaamini yatawasaidia kuibuka na ushindi na kutinga fainali.

Alisema mara nyingi timu hizo zinapokutana mchezo huwa mgumu na ushindani mkubwa kutokana na aina ya timu, lakini hawana wasiwasi kuhusu kuibuka na ushindi.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >